# Nipashe

Jumamosi Julai 4, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580275

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN

215779502




## Mwanasiasa mashuhuri Njelu Kasaka wa G-55 afariki dunia

UKURASA 3

# Askofu Shoo aomba radhi



UKURASA 2



### BAA LA CORONA

**Utafiti unaonyesha kuwa watoto na vijana wanaweza kupata maambukizi ya virusi vya corona na kuambukiza wengine kama yalivyo makundi mengine. 'Usichukulie poa unategemewa'. WHO**

- **Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka**
- **Kaa kwa kuachiana nafari hatua 2 au 3**
- **Vaa barakoa**
- **Ukikohoa au kupiga chafya ziba mdomo**

## Mbaroni kukutwa na doti 600 CCM

UKURASA 2




Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga, Hussein Mussa, akionyesha doti 600 za vitenge vyenye nembo ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambavyo vimekamatwa kutoka kwa mfanyabiashara wa usafiri wa magari madogo (TAXI), Johas Tasia, vikiwa nyumbani kwake, eneo la Mwasele, mjini Shinyanga, kwa madai ya kutumika kushawishi wapigakura ndani ya chama hicho. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Majibu ya TAKUKURU hoja 10 za CHADEMA

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store



MICHEZO MECHI CHUNGU YANGA LIGI KUU UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

## Mfanyabiashara abambwa na doti

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Shinyanga, imemkamata mfanyabiashara wa magari ya teksi, Joseph Tasia, akiwa na doti 600 za vitenge vyenye nembo ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) nyumbani kwake na kushindwa kutoa maelezo yanayojitosheleza.

Mkuu wa Takukuru mkoani humo, Hussein Mussa, katika taarifa yake jana alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Juni 29, saa 3:00 usiku mtaa wa Mwasele B.

Mussa alisema walimkamata Tasia akiwa na doti hizo zikiwa zimehifadhiwa nyumbani kwake jambo ambalo linaashiria kuwa zilikuwa zinaandaliwa kutumika katika kufanya ushawishi kwa wapigakura.

"Uchunguzi wa Takukuru mkoani Shinyanga umebaini Tasia mfanyabiashara wa magari madogo ya teksi hana duka wala hafanyi biashara ya kuuza vitenge," alisema.

Aidha, alisema katika mahojiano alishindwa kutoa maelezo yanayotosheleza kuhusiana na mzigo huo aliokutwa nao na hata nyaraka za ununuzi alizowasilisha hazijitoshelezi, hivyo kuonyesha shaka juu ya uhalali wake.

"Uchunguzi wa kina wa tukio hili unaendelea ili kubaini iwapo vilikuwa kwa ajili ya kuhusiana na vitendo vya rushwa katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, mwaka huu au ni kwa ajili ya kufanya biashara katika msimu huu," alisema.

# Askofu Shoo aomba msamaha

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amewaomba msamaha Watanzania waliougulikwa na kupoteza ndugu, jamaa na marafiki kwa ugonjwa wa corona kutokana na kunyanyapaliwa na kukimbiwa na baadhi ya madaktari, wauguzi na viongozi wa kanisa.

Vilevile, kiongozi huyo wa kanisa ametoa msaada wa vifaa kinga na dawa vyenye thamani ya Sh. milioni 100 kwa hospitali 24 nchini zinazomilikiwa na kanisa hilo, ili ziendelee kutoa huduma stahiki kwa wagonjwa wa corona na kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi hivyo.

Akizungumza jijini Arusha jana, wakati akikabidhi msaada huo kwa wawakilishji wa hospitali hizo nchini, alishukuru Shirika la Kimataifa la Act Alliance kwa kutoa fedha zilizowezesha kununua vifaa tiba kwa ajili ya kukinga madaktari na wauguzi pamoja na dawa za aina mbalimbali za kukabiliana na corona na magonjwa mengine.

Askofu Shoo alisema binadamu wote wanastahili huduma za kibinadamu na kuzikwa kwa heshima hata kama amefariki dunia kwa ugonjwa hatari, hivyo waliokumbwa na unyanyapaa wa aina yoyote, anawaomba msamaha kwa niaba ya kanisa. Alishauri hospitali zote nchini kujiweka tayari kukabiliana na majanga ya magonjwa yoyote yanapotokea kama corona kwa kuwa na vifaa mbalimbali vya kuhudumia Watanzania.

Dk. Shoo pia alitoa wito kwa serikali kuwatafuta na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wale wote wanaojihusisha na ukatili dhidi ya watoto katika familia na majumbani hasa wanafunzi wanaopewa mimba na kukatishwa ndoto zao.

Aliwashauri viongozi wa dini wawe mstari wa mbele kuwafariji na kuwapa ushauri nasaha wale wote walioathrika na corona, kwa kuwa ugonjwa huo bado upo na kila mmoja anapaswa kuchukua tahadhari zote kama inavyoshauriwa na wataalamu wa afya na serikali.

"Niwatie moyo wafanyabiashara ambao mitaji yao imeyumba wakati wa corona, kwamba sasa hali yetu inaelekea kurejea kama kawaida, ninawaombea kwa Mungu awainue upya waendelee na biashara zao kwa nguvu na kuujenga uchumi wetu na familia zao," alisema.

Aliwapongeza madaktari na wauguzi kwa kufanya kazi wakati huo mgumu wa janga la corona, huku baadhi yao wakipata vikwazo vya kutolipwa mishahara yao.

Dk. Shoo pia alimpongeza Rais John Magufuli kwa kuongoza vema serikali yake na kufanikiwa kutangazwa na Benki ya Dunia kuwa Tanzania sasa imefikia uchumi wa kati.

"Rais alipoingia katika serikali hii, alisema Watanzania tufanye kazi, ili tufikishe taifa katika uchumi wa kati, lakini katika hili baadhi ya watu walibeza kuwa haiwezekani na kusema ni ndoto, lakini limewezekana na Benki ya Dunia imetutangaza rasmi kuingia katika uchumi wa kati, ninampongeza sana Rais," alisifu.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa (wa pili kushoto), wakipata maelezo ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Benki ya CRDB kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela (wa pili kulia), kabla ya kufungua maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja wa Benki hiyo, Kanda ya Mashariki, Badru Idd. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majibu ya TAKUKURU hoja 10 za CHADEMA

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imejibu hoja 10 za Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kuhusu chama hicho kutokuwa na imani na uchunguzi unaofanywa na taasisi hiyo dhidi yake.

Mwezi uliopita, TAKUKURU ilitangaza kuanza uchunguzi kuhusu tuhuma za matumizi mabaya ya michango ya wanachama wa CHADEMA, wakiwamo wabunge wake wanaokatwa sehemu ya mishahara yao ili kutunisha mfuko wa chama.

Hata hivyo, juzi, CHADEMA kupitia kwa Katibu Mkuu wake, John Mnyika, ilisema haina imani na uchunguzi unaoendelea kufanywa na taasisi hiyo dhidi yake kutokana na kauli alizoziita za kisiasa zilizotolewa na uongozi wa juu wa TAKUKURU kuhusiana na uchunguzi huo.

Mnyika alisema taasisi hiyo tayari imeshawahoji watu 60, wakiwamo viongozi na wanachama wa CHADEMA huku pia wakiikabidhi nyaraka kadhaa zinazohusiana na fedha za michango ya wabunge wa chama hicho.

Mnyika alidai uchunguzi huo unafanywa kisiasa kwa lengo la kuichafua CHADEMA kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu, huku akisisitiza kwamba hadi sasa TAKUKURU haijaweka wazi ukomo na aina ya tuhuma ambazo zinaikabili CHADEMA.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Ofisa Uhusiano wa TAKUKURU, Doreen Kapwani, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wake, Brigedia Jenerali John Mbungo, alijibu hoja 10 za chama hicho.

Alianza kujibu hoja ya CHADEMA kutokuwa na imani na uchunguzi wa TAKUKURU, akisema taasisi hiyo ni chombo cha uchunguzi kilichoundwa na kupewa mamlaka ya kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Kapwani pia alisema TAKUKURU ni chombo chenye wataalamu waliobobea katika shughuli za kiuchunguzi na kamwe hakiwezi kuelekezwa namna ya kufanya uchunguzi dhidi ya tuhuma za rushwa na watu ambao kinawachunguza. "Hiki ni chombo huru kwa mujibu wa kifungu cha 5(2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007," alisema.

Kuhusu hoja ya ukomo wa uchunguzi, Kapwani alifafanua kuwa kitaaluma, suala la uchunguzi huwa halina mipaka wala ukomo, hivyo wakichunguza jambo moja, hawawezi kuzuiwa kuchunguza jambo lingine linalojitokeza katika uchunguzi huo.

Kapwani alisema CHADEMA wanapaswa kutulia na kusubiri matokeo ya uchunguzi kwa sababu kupitia uchunguzi wowote, ukweli hujulikana na uongo hubainika.

Kuhusu taasisi kutumika kisiasa, Kapwani alisema hoja hiyo haina msingi kwa kuwa TAKUKURU ni chombo huru kinachotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na mamlaka yake ni kuchunguza bila ubaguzi wowote wa rangi, dini, kabila, chama, jinsi, umri wala elimu.

Alisema inafahamika kuwa CHADEMA ndiyo chama kilichosimama bungeni kupitia wabunge wake na kutoa malalamiko dhidi ya matumizi mabaya ya fedha za michango yao na ubadhirifu ni kosa la jinai. "Malalamiko yale yalikuwa ni chanzo cha taarifa kwa TAKUKURU na hata kama suala kama hilo lingetokea kwa chama kingine chochote, taasisi ingefanya hivyo hivyo," alisema.

HABARI KITAIFA

# Mwanasiasa Njelu Kasaka afariki dunia

**Na Mwandishi Wetu**

MWANASIASA mkongwe nchini aliyewahi kushika nyadhifa mbalimbali katika taasisi za umma na serikalini, Njelu Kasaka, amefariki dunia.

Masache Kasaka, mtoto wa marehemu, aliliambia gazeti hili kwa simu kuwa Kasaka (78) alifariki dunia usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Rufani ya Kanda, Mbeya alikokuwa anapatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa Masache, Kasaka alifikishwa hospitalini hapo kutoka Chunya baada ya kuugua ghafla Ijumaa iliyopita alipokuwa katika shughuli zake huko.

“Ni kweli baba amefariki (dunia) usiku wa kuamkia leo (jana) na hivi tunavyoongea msiba uko hapa nyumbani kwangu Mbeya mjini. Leo (jana) tunatarajia kusafirisha mwili wa mzee wetu kwenda nyumbani Chunya. Tunatarajia kumzika baba Jumapili (kesho),” alisema Masache.

Kasaka alikuwa Mbunge wa Chunya na baadaye Lupa kuanzia mwaka 1990 hadi 2005. Katika kipindi cha ubunge wake, Kasaka alijipatia sifa kutokana na kuongoza kundi la wabunge 55, maarufu kama G-55, ambalo liliibua vuguvugu la kudai serikali ya Tanganyika mwaka 1993.

Kabla ya kuwa mbunge, alikuwa mtumishi katika iliyokuwa Benki ya Maendeleo Vijijini (TRDB) ambayo ilibadilishwa na kuwa Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (CRDB) katika mikoa ya Kilimanjaro, Mtwara, Iringa na makao makuu, Dar es Salaam.

Katika kipindi cha ubunge, aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Kilimo mwaka 1994 hadi 1996 kabla ya kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa na baadaye Tabora.

Sambamba na nafasi hizo, mwaka 2001 hadi 2005 alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Mipango ambayo pamoja na mambo mengine ilisimama kidete katika ubinafsishaji wa Benki ya National Microfinance (NMB).

Kasaka ambaye ameacha mjane na watoto wanane, alizaliwa mwaka 1942 Chunya mkoani Mbeya. Alikuwa msomi katika fani ya uchumi ambapo alipata shahada ya kwanza ya uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) mwanzoni mwa miaka ya 1970 na shahada ya pili katika Uchumi Kilimo aliipata Chuo Kikuu cha Kentucky, Marekani.

# Adengenye RC Kigoma, Mwanri astaafu Tabora

**Na Mary Geofrey**



RAIS John Magufuli amefanya uteuzi wa wakuu wa mikoa miwili, akimteua aliyekuwa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma kuchukua nafasi ya Brigedia Jenerali mstaafu Emmanuel Maganga ambaye amestaafu.

Januari 23, mwaka huu, Rais Magufuli alitengua uteuzi wa Andengenye na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, kutokana na mkataba mbovu ambao jeshi hilo liliingia na Kampuni ya Romania kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbalimbali.

Hata hivyo, mapema mwezi uliopita, Rais Magufuli wakati akizindua Jengo la Jeshi la Magereza mkoani Dodoma, alitangaza kumsamehe Andengenye kwa maelezo kuwa kiongozi huyo alikuwa akimwomba msamaha mara kadhaa.

Rais Magufuli alitangaza uteuzi huo jana jijini Dodoma, akiteua pia wakuu wa wilaya tisa nchini ambao wanatarajiwa Jumatatu Julai 6 mwaka huu.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, Rais Magufuli amemteua Dk. Philemon Sengati kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora.

Dk. Sagati ambaye alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, anachukua nafasi ya Aggrey Mwanri (pichani) ambaye amestaafu.

Kuhusu wakuu wa wilaya tisa, taarifa hiyo ilieleza kuwa, Rais Magufuli amemteua Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza Ismail Mlawa, kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro.

Kabla ya uteuzi huo, Mlawa alikuwa Mkuu wa Magereza wa Mkoa wa Morogoro na amechukua nafasi ya James Ihunyo ambaye amestaafu.

Taarifa hiyo ilieleza zaidi kuwa, Rais Magufuli amemteua Jamila Yusuf kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi. Kabla ya uteuzi huo, Jamila alikuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma na anachukua nafasi ya Lilian Matinga ambaye amestaafu.

Rais Magufuli pia amemteua Martine Ntemo kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani. Awali alikuwa Mhandisi katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na anachukua nafasi ya Asumpter Mshama ambaye amestaafu.

Vilevile, Rais Magufuli amemteua Salum Kali kuwa Mkuu wa Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, ambaye kabla ya uteuzi, alikuwa Katibu wa CCM Mkoa wa Mwanza na anachukua nafasi ya Dk. Philemon Sengati ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora.

Mwingine aliyeteuliwa ni Wilson Shimo ambaye anakuwa Mkuu wa Wilaya ya Nyang’wale mkoani Geita. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Singida.

Rais Magufuli pia amemteua Kanali Mathias Kahabi, kuwa Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera, akichukua nafasi ya Saada Malunde ambaye amestaafu.

Taarifa hiyo pia ilieleza kuwa, Rais Magufuli amemteua Abbas Kayanda kuwa Mkuu wa Wilaya ya Karatu mkoani Arusha. Kabla ya uteuzi, alikuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Karatu na anachukua nafasi ya Theresia Mahongo ambaye amestaafu.

Uteuzi mwingine ni wa Lazaro Twange ambaye anakuwa Mkuu wa Wilaya ya Babati mkoani Manyara. Twange anachukua nafasi ya Elizabeth Kitundu ambaye amestaafu.

Rais Magufuli pia amemteua Toba Nguvila kuwa Mkuu wa Wilaya ya Handeni. Kabla ya uteuzi, alikuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Longido mkoani Arusha.

Nguvila anachukua nafasi ya Godwin Gondwe ambaye amehamishwa kituo cha kazi na kuwa Mkuu wa Wilaya ya Temeke mkoani Dar es Salaam, kuchukua nafasi ya Felix Jackson aliyestaafu.

“Uteuzi wa viongozi hao umeanza leo (jana) Julai 3, mwaka huu na wateule wote wanatakiwa kuwapo Ikulu, Chamwino mkoani Dodoma Julai 6 saa 4:00 asubuhi,” ilielezwa katika taarifa hiyo ya Ikulu.


**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collection Auctioneer, Commission Agent & Legal Consult

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC** tutauza kwa **MNADA WA HADHARA,** dhamana za wadaiwa. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea mahali dhamana zilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

| No | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA | TAWI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SALOME BENNY MLANZI/DEBORA ALLY MMANGA | Nyumba iliyopo Luguruni kwembe yenye Hati ya mauziano yenye jina la Debora Ally Mmanga | 31/7/2020 | UBUNGO |
| 2 | Alphani Jafari Juma | Nyumba ya makazi yenye hati ya mauziano iliyopo kibaha Mkoa wa pwani eneo la miembe saba B. | 25/7/2020 | UBUNGO |
| 3 | Bashiru Yasini Adolf | Nyumba yenye hati ya mauziano iliyopo Chanika | 22/7/2020 | UBUNGO |
| 4 | Jackson Damas Mauki/Jackenn Bro’s company | Nyumba yenye hati ya mauziano iliyopo eneo la Stop over inayomilikiwa na Jackson Damas Mauki | 17/7/2020 | TEGETA |
| 5 | Salum kondo Mwinyimkuu | Nyumba yenye leseni ya makazi na. KND006783, ardhi na.KND/TND/MHT4/34 Iliyopo mtaa wa Muhalitani kata ya Tandale manispaa ya Kinondoni | 18/7/2020 | UBUNGO |
| 6 | Hadija Hassan Mwasha | Nyumba ya makazi yenye leseni na KND15443, ardhi na.KND/MBS/KWN26/175 mtaa wa kisiwani Mwananyamala manispaa ya Kinondoni. | 18/7/2020 | TANDALE |
| 7 | Happyness Daniel Rwehumbiza/Daudi Mussa Sunta | Nyumba yenye Hati ya mauziano iliyopo mbezi msumi | 17/7/2020 | UKONGA |
| 8 | Masudi Jumanne Ramadhani/Beatrice stephano kisheru | Nyumba yenye Hati ya mauziano iliyopo Temboni Saranga | 31/7/2020 | UKONGA |
| 9 | Sophia Salum Nkiya | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano iliyopo<br>1.Kipala -Mkurangamkoa wa pwani<br>2.Mbezi Msumi | 24/7/2020 | UKONGA |
| 10 | Bethsaida enterprises/Venance Victoria kadea | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano iliyopo maeneo ya Vikongoro Chanika | 29/7/2020 | UKONGA |
| 11 | Yakobo Ayubu Hambije | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano iliyopo maeneo ya Zavara | 22/7/2020 | UKONGA |
| 12 | Mwajuma Hamisi Amani/Justini Gerade Kimario | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano iliyopo maeneo ya Vikongoro Chanika | 29/7/2020 | UKONGA |
| 13 | Meshack Willy Kweka | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano iliyopo maeneo ya Kilungule inayosomeka kwajina la Meshack Willy Kweka | 29/7/2020 | UKONGA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Akiba Commercial Bank PLC,**
**P.O. BOX 699,**
**DAR ES SALAAM.**
**Tel: +255 022 211 8340-3**

215799702

# Tigo yadhamini tena Sabasaba

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mawasiliano ya Tigo Tanzania, kwa mwaka wa tano mfululizo, imekuwa mdhamini mkuu wa mawasiliano kwenye maonyesho ya kimataifa ya biashara, marufu kama Sabasaba.

Maonyesho hayo ambayo yalifunguliwa rasmi jana na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kwa mwaka juu yanabeba kaulimbiu isemayo 'Uchumi wa Viwanda kwa Ajira na Biashara Endelevu'.

Kutokana na kaulimbiu hiyo, taarifa iliyotolewa jana na Tigo ilisema kampuni hiyo wakati wa maonyesho hayo, itaonyesha bidhaa na huduma ambazo zina mchango mkubwa katika kuhakikisha uchumi wa viwanda unafikiwa..

Meneja wa Mawasiliano wa Tigo Tanzania, Woinde Shisael, alisema katika taarifa hiyo kuwa alisema Tigo imekuwa mbia mkubwa wa maonyesho hayo katika kipengele cha mawasiliano kwa mwaka wa tano mfululizo.

Alisema ushirikiano huo unaonyesha Tigo ilivyojizatiti katika kuunga mkono juhudi za serikali za kuinua biashara pamoja na ukuaji wa viwanda vya ndani ili kuongeza pato na uchumi wa taifa.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ambao ni waandaaji wa maonyesho hayo, Theresa Chilambo, aliipongeza na kuishukuru Tigo kwa udhamini huo.

Chilambo alisema TanTrade inajivunia kuwa na mbia wa kuaminika katika kipengele cha mawasiliano na kwamba mamlaka iko tayari kushirikiana kikamilifu na Tigo kwenye maonyesho ya mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Tigo imeingia ubia na kampuni zinazouza simu za mkononi ili kutoa ofa kabambe ikiwamo huduma za intaneti na promosheni za simu janja kwa maelfu ya wateja watakaoudhuria

# Ajali ya Noah, lori ilivyoua watano

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU watano wamekufa na wengine wawili kujeruhiwa katika ajali ya barabarani iliyohusisha gari aina ya Noah lenye namba za usajili T 897 DCC na lori aina ya Scania lenye namba za usajili T 183 AXC.

Ajali hiyo ilitokea jana majira ya saa 11:30 alfajiri eneo la Kibaigwa wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika eneo la tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa lori aliyeingia barabarani bila kuchukua tahadhari.

"Mpaka sasa ninapozungumza, tayari watu watano wamepoteza maisha, akiwamo dereva wa gari dogo aina ya Noah, Yohana Ndugai, (34), na wengine wawili ni majeruhi, ambapo mmoja wao yuko mahututi," alisema.

Kamanda Muroto alisema dereva wa lori aina ya Scania lililokuwa likitokea Dodoma kwenda Morogoro, ndiye mwenye makosa kutokana na kuingia barabarani bila kuchukua tahadhari, na kwamba mara tu baada ya kutokea kwa ajali hiyo, alikimbia na Jeshi la Polisi linaendelea kumtafuta.

"Huyu dereva, yeye alitumwa kuja huku Dodoma kuleta 'spea', lakini kutokana na tamaa, alipakia na watu wengine kama abiria ambao baadhi yao ndiyo waliohusika katika ajali hii.

"Hivyo basi, nitoe wito kwa madereva kuhakikisha kuwa wanazingatia sheria za usalama barabani," Kamanda Muroto alisema.

Alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma litaongeza usimamizi mkali kwa madereva wote wanaovunja sheria hasa katika kipindi hiki ambacho Mkoa wa Dodoma, unakwenda kupokea wageni wengi kwa ajili ya mkutano mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mwezi huu.

"Ninafikiria sasa madereva wameshaanza kuleta uzembe ambao tulikuwa tunaupigia kelele, kwa sababu katika ajali hii huyu dereva ameingia bila kuchukua tahadhari na pia hajaheshimu gari lingine kutokana na yeye kuwa na lori kubwa, ndiyo maana hakumheshimu mwenye Noah," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejebi, akiwa katika tukio hilo, alisema: "Tunashukuru Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma, kwa kazi waliyoifanya kwani wamefika katika eneo la tukio kwa wakati, hali ambayo imesaidia hata barabara hii kuendelea kupitika pamoja na kuwa lori hili baada ya kupata ajali, liliziba sehemu ya barabara," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, akizungumza katika ajali hiyo, aliitaka Jeshi la Polisi kuendelea kumtafuta dereva wa lori aliyesababisha ajali hiyo na kukimbia.

"Lakini pia nitoe angalizo kwa madereva kuhakikisha kuwa wanakuwa makini wakati wote wanapoendesha vyombo vya moto, kwani wamepakia roho za binadamu, ni lazima wawe makini kila wakati ili kuondokana na uzembe kama huu," aliagiza.

Kiongozi huyo wa mkoa pia aliwaagiza wakurugenzi wa Wilaya za Chamwino, Kongwa na Bahi, kuhakikisha malori yote yanayoegeshwa katika maeneo ya barabara, yanaacha kufanya hivyo mara moja.

"Tulikubaliana katika kikao cha ushauri mkoa (RCC) kuwa katika eneo la Kibaigwa, Chalinze nyama na Bahi malori hayatakiwi kuendelea kuegeshwa katika maeneo ya barabara, bali wakurugenzi watafute maeneo maalum kwa jili ya kuegesha malori, ili kuondokana na ajali kama hizi za kizembe," alikumbusha.



Wananchi wakishuhudia mabaki ya gari aina ya Noah yenye namba za usajili T 897 DCC, baada ya kugongana na Lori aina ya Scania lenye namba za usajili T183 AXC, katika eneo la Kibaigwa wilayani Kongwa, mkoani Dodoma jana, na kusababisha watu watano kufariki dunia na wawili kujeruhiwa. **PICHA: PAUL MABEJA**

# 'Undeni vikundi tuwape mikopo ya halmashauri'

**Na Steven William,** MUHEZA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga. Nassibu Mmbaga, amewataka wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kujitokeza kwa wingi kuunda vikundi, ili wapate mikopo ya fedha zinazotolewa na halmashauri.

Alitoa rai hiyo juzi, alipozungumza na baadhi ya vikundi vilivyopata mkopo hiyo ambayo ni asilimia 10 ya mapato ya halmashauri.

Alisema kuwa mkopo wa halmashauri hauna riba, akiwataka vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kujitokeza kwa wingi kuchukua mikopo, ili wanufaike na fedha hizo kwa kufanya miradi.

Mmbaga alivitaka vikundi vinavyopata mikopo hiyo virejeshe kwa wakati, ili fedha hizo zisaidie makundi mengine.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Muheza, Shabani Maghembe, alisema kuwa wanavikundi ambao watakopa, ni lazima warejeshe fedha mapema ili kuruhusiwa kukopa tena.

Alisema mikopo hiyo kwa mwaka inatoka mara mbili na kwamba sasa wanakikundi hao wanatakiwa wakafanye kazi kubwa, ili waanze kurejesha mapema.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Muheza, Vije Mfaume, alibainisha kuwa kwa mwaka 2019/2020, halmashauri ya Muheza ilitenga Sh. milioni 248 kwa ajili ya mikopo kwa vikundi vya uzalishaji mali vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Alisema Sh. milioni 130.341 zilikuwa zimetolewa hadi Aprili mwaka huu kwa vikundi 24 na kwa robo ya nne (Aprili hadi June mwaka huu), halmashauri imetenga Sh. milioni 116.8 kwa ajili ya kukopesha makundi hayo.

# Ukaguzi vipimo wa kushtukiza wakomboa wakulima

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo Mizani (WMA) umesema ukaguzi wa kushtukiza ambao umekuwa ukifanya nchi nzima mara kwa mara, uzimesaidia kwa kiasi kikubwa wakulima kutoibiwa na wafanyabiashara wasio waaminifu.

Meneja wa WMA Kitengo cha Bandari, Peter Chuwa, alisema jana kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Alisema wamekuwa wakifanya kaguzi za mizani kila baada ya miezi 12 na kukuta baadhi ya mizani imechezewa na wafanyabiashara hao kwa lengo la kuwaibia wakulima wa mazao mbalimbali kama korosho na pamba na ndiyo sababu wameamua kuwashtukiza.

Alisema WMA imesambaza namba za simu za bure ambazo wakulima na watu mbalimbali wanaohisi kupunjwa vipimo kuwapigia na maofisa wake kwenda kwa ajili ya kuwakamata wahusika na kuwachukulia hatua za kisheria kama kulipa faini.

Chuwa alisema ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara umesaidia kwa kiwango kikubwa kuwabaini wafanyabiashara wanaochezea mizani na wamekuwa wakitozwa faini kwa mujibu wa sheria.

"Hawa wafanyabiashara wakisikia WMA inaenda wanaweka mambo sawa na wala hamuwezi kukuta mzani uliochezewa lakini hizi kaguzi za kushtukiza zimesaidia sana kuwakamata na imepunguza hali ya kucheza na mizani mara kwa mara," alisema

"Kuna watu wananamba zetu wamekuwa wakitupigia na wakati mwingine tunapata malalamiko kwa watu kupunjwa vipimo au WMA inapohisi kuna sehemu mambo hayako sawa sawa tunaenda kwa kushtukiza na kuwanasa wahusika," alisema

Alisema wamekuwa wakienda kwenye viwanda vya nondo, tiles, maji, viwanda vya saruji kupima kama bidhaa wanazotengeneza zinawekwa vipimo sahihi kama walivyotangaza kwenye makasha yao.

"Mtu akisema hii nondo ni milimita 12 lazima tupime tujiridhishe kwamba ni milimita 12 na mfuko wa saruji unaandikwa kwamba una kilo 50 lazima tupime kama kweli ni kilo 50 na tuko makini kufanya hivyo kumlinda mlaji apate anachostahili," alisema Chuwa.

Kaimu Meneja sehemu ya ukaguzi na ufuatiliaji, Almachius Pastory, alisema wamekuwa wakitoa elimu na kufanya kaguzi za kutosha kwenye mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita, Mara, Shinyanga na Kagera ili kuwalinda wakulima wa pamba wasiibiwe na wafanyabiashara wasio waaminifu.

Alisema elimu inayotolewa WMA imewezesha wakulima kujua vipimo sahihi wanapouza mazao yao na wameachana na tabia ya zamani ya kuuza mazao yao kwa kutumia vipimo batili.

"Hali hii imepunguza kwa kiwango kikubwa wanunuzi vishoka ambao wanawarubuni wakulima na wengi wamehamasika kuuza mazao yao katika vyama vya msingi na kunufaika na bei nzuri inayopangwa na serikali," alisema

# Waziri Mkuu: Watanzania tununue bidhaa za ndani

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI Mkuu Kassimu Majaliwa, amewataka Watanzania kununua bidhaa zinazozalishwa nchini, ili kukuza viwanda vya ndani na kuuinua zaidi uchumi wa nchi.

Majaliwa alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam alipokuwa anafungua Maonyesho ya 44 ya Kimataifa ya Biashara, maarufu Sabasaba, yakiwa na washiriki 2,880 wa ndani na nje ya nchi walioijitokeza kuonyesha bidhaa zao.

Alisema serikali inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha bidhaa za ndani zinaboreshwa sambamba na kuboresha mazingira ya uzalishaji wa bidhaa hizo nchini.

Alisema serikali itaendelea kuongeza kodi kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi, ili bidhaa za ndani zipate soko la uhakika.

"Muhimu kwetu ni kuhakikisha tunasimamia maendeleo yetu na kutatua matatizo yanayowakabili wafanyabiashara wa ndani na hivyo kuzalisha na kupata masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema.

Majaliwa alizitaka taasisi zinazojihusisha na utafiti, ziendelee kufanya kazi yake, ili kuwa na suluhisho la kudumu la matatizo yanayozikabili bidhaa za ndani.

Mtendaji mkuu huyo wa shughuli za serikali alipongeza jitihada zilizokuza sekta ya sanaa, burudani na michezo nchini, akibainisha kuwa sekta hiyo kwa sasa inatisha kwa kasi ya ukuaji nchini.

Katika hatua nyingine, Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), limepeleka huduma yake ya 'T-Burudani' katika maonyesho hayo.

Meneja Uhusiano wa shirika hilo, Puyo Nzalayaimisi, alisema jana kuwa, Watanzania watakaotembelea maonyesho ya mwaka huu ndani ya banda lao, watajipatia huduma ya T-Burudani yenye ofa ambayo inatamwezesha mteja kupakua, kuhifadhi na kuangalia filamu aipendayo hata bila ya kuwa na mtandao wa intaneti.

Aliwaomba wananchi hasa wapenzi wa filamu nchini, kufurahia ofa hiyo ya Sh. 2,000 na kujipatia huduma ya T-Burudani toka TTCL itakayowezesha mteja kuangalia filamu na tamthilia aipendayo bila ya kuwa na mtandao wa intaneti.

"Huduma ya T-Burudani ya TTCL ni rahisi, inamwezesha mteja kupakua filamu bila kutumia kifurushi cha intaneti, mteja ataweza kuangalia filamu zote za ndani ya nchi na kimataifa, mteja ataweza kupakua kupitia simu janja ya mkononi pamoja na kompyuta ya kiganjani," alisema.

Nzalayaimisi alisema TTCL imeweka mfumo rahisi utakaomwezesha mteja kupakua filamu aitakayo kutokana na maudhui anuai duniani ikiwa ni pamoja na Hollywood, Nollywood, Bollywood, HBO, na Bongo Movies.

Aliongeza huduma nyingine ambazo TTCL inazitoa katika viwanja vya Sabasaba ni pamoja na huduma za usajili laini kwa wateja, kurudisha laini zilizopotea, vifaa vya internet kama modem na vinginevyo, huduma za T-PESA, huduma za mkongo wa taifa wa mawasiliano na huduma za Data Senta.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, akitoa maagizo mbalimbali kwenye banda la Wakala wa Vipimo (WMA), kwenye maonyesho ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Kaimu Meneja Ukaguzi na Ufuatiliaji wa wakala hiyo, Almachius Pastory na Meneja wa Mawasiliano wa WMA, Irene John. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri: Huduma za hoteli ziboreshwe

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, amewataka watoa huduma za hoteli za kawaida na za kitalii nchini, kuhakikisha wanaendelea kuboresha utoaji wa huduma kwenye maeneo yao, ili kuwavutia wageni.

Constatine Kanyusu alitoa rai hiyo jana wakati wa hafla ya kutoa daraja za nyota kwa hoteli zilizopangwa kutokana na ubora kwa mkoa wa Dodoma.

Aliwataka watoa huduma za hoteli nchini kuhakikisha wanaendelea kuboresha utoaji wa huduma kwenye maeneo yao ili kuwavutia wageni na kukuza kipato chao na taifa kwa ujumla.

"Ninatoa wito kwa watoa huduma wote wa hoteli za jijini Dodoma na nchi nzima kwa ujumla, kuendelea kuboresha utoaji wa huduma katika maeneo yenu, ili kuwavutia watalii na wageni wa kawaida," alisema.

Alisema moja ya majukumu ya wizara hiyo ni kupitia Sheria ya Utalii Na. 29 ya Mwaka 2008 na kupanga huduma za malazi katika madaraja ya ubora kwa mfumo wa alama za nyota unaotumika katika ubora wa huduma.

Kanyasu alibainisha kuwa ubora huo unaandaliwa na kutumika katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kulingana na vigezo ambapo hoteli zenye ubora wa juu hupewa daraja la tano na kiwango cha chini hupewa daraja la nyota moja.

Hata hivyo, alisema hoteli ambazo hazijafikia kiwango cha daraja la nyota, hutambulika kama huduma za malazi zilizothibitishwa kimataifa.

Alisema sekta ya utalii nchini imeendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya nchi ambapo mwaka 2019 iliingizia taifa Dola za Marekani milioni 2,612.9.

Alitaja idadi ya watalii waliotembelea katika mwaka huo kuwa ni 1,527,230 na kutoa ajira milioni 1.5 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Kanyasu alisema ongezeko la watalii nchini, litahitaji kwenda sambamba na kuboresha huduma zitolewazo katika sekta hiyo.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Profesa Adolf Mkenda, alisema kazi ya uhakiki ilianza mwaka 2018 ambapo katika mkoa wa Dodoma, jumla ya hoteli 428 za utoaji huduma za malazi zilihakikiwa.

Profesa Mkenda alibainisha kuwa katika mkoa huo, hoteli 24 tu ndiyo zilizokidhi vigezo vya ubora wa utoaji huduma kwa vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki vya upangaji wa madaraja ya ubora.

Alisema kati ya hizo, hoteli 11 zimepata alama za daraja la nyota na nane hazijafikia, lakini zimepewa hadhi ya hoteli zinazotambulika na tano hazijakidhi vigezo mahsusi vilivyowezesha kupangwa kwenye madaraja ya ubora.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Klabu, wachezaji muhimu kuheshimu mikataba yenu

**LIGI** Kuu Tanzania Bara iko katika hatua za lala salama au kwa maneno mengine unaweza kusema inaelekea ukingoni.

Ligi hiyo inayoshirikisha timu 20 kutoka mikoa mbalimbali, ndio ya juu kwa upande wa Bara na hutoa tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambayo husimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Pia kuna mashindano ya Kombe la FA ambayo huanza katika ngazi za wilaya na bingwa wa michuano hii kupeperusha bendera ya Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa upande wa Visiwani, huko kuna Ligi Kuu Zanzibar ambaye bingwa wake hukiwakilisha kisiwa hicho kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na mshindi wa Kombe la FA huenda katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, kwa sababu wao pia ni wanachama wanaotambulika kwenye ngazi klabu.

Ili timu zetu za Tanzania ziweze kufanya vizuri katika mashindano hayo ya kimataifa, ni lazima wachezaji wa klabu zitakazopata nafasi ya kwenda kuchuana kwenye michuano hiyo, kuandaliwa vema. Maandalizi ya wachezaji yanatakiwa kufuata taratibu zote muhimu kuanzia katika hatua ya kwanza ya mazungumzo yanayopelekea kukamilisha kwa mchakato wa usajili.

Mchakato huo wa usajili ndio huzalisha uhusiano mzuri kati ya viongozi na wachezaji kwa kila upande kutakiwa kutekeleza vipengele vilivyowekwa kwenye mkataba unaosainiwa na endapo itaenda tofauti, mambo huharibika katikati ya safari.

Nipashe inawakumbusha viongozi wa klabu, wachezaji na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuhakikisha mikataba yote inayoingiwa kati ya klabu na wachezaji inalindwa kwa ajili ya maslahi ya pande zote mbili. Kama TFF ambao ndio wasimamizi wakuu wa soka hapa nchini, hawatakuwa makini kuwatetea wachezaji au klabu zake, basi kila siku tutaendelea kushuhudia 'mauzauza' kati ya pande mbili hizo na hatimaye klabu husika kuathirika kwa kutoka huduma ya mchezaji.

Mara nyingi msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara ukiwa unaelekea ukingoni, tumeshuhudia klabu zikikimbiwa na wachezaji wake kwa madai ya kutowalipa sehemu za fedha za usajili zilizobaki au kutolipwa mishahara. Hali hii huathiri matokeo ya timu iwe katika mbio za kuwania ubingwa au kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Tufike wakati viongozi wa klabu na wachezaji kila mmoja akatekeleza majukumu yake na hapo tutashuhudia mipango na mikakati ya makocha katika kuwania mataji ikafanyika bila changamoto, lakini itakwama pale atakapowakosa wachezaji aliowatarajia kwa sababu ya sintofahamu au migogoro ya mikataba. Nidhamu na kiwango bora cha mchezaji huanzia kwenye ngazi ya klabu, huu ni wakati mwingine wa TFF kuwaandalia elimu wachezaji ili wafahamu majukumu yao na baadaye watakapoitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), wawe imara na kuisadia nchi kufanya vema katika mashindano wanayoshiriki.


Ili kujiepusha na migongano hii, TFF inawasisitiza wachezaji wote wanaocheza soka hapa nchini kutumia mawakala waliosajiliwa na shirikisho hilo ambao watawasaidia kulinda maslahi yao wakati wanaposaini au wanapotaka kuvunja mikataba.

Gazeti hili linawakumbusha wachezaji kutoogopa gharama za kuwatumia mawakala, kwa sababu wananafasi kubwa ya kumaliza matatizo ya kimkataba kutokana na uelewa walionao na hapo itawaweka kwenye nafasi salama pale watakapokuwa wanadai stahili zao.

Tunawashauri viongozi wa timu kuacha kufanya mazungumzo na wachezaji wakiwa peke yao kwa kuangalia zaidi maslahi ya klabu, lakini wakumbuke tofauti zozote za makubaliano zinapotokea huanza kuziumiza timu kwa kutokana na hatua ya awali ya mchezaji kugoma kuitumikia klabu yake.

Tubadilike, wachezaji, viongozi chini ya usimamizi wa TFF, fanyeni taratibu za usajili kisasa ili mwisho wa siku kila upande ufaidike na makubaliano yaliyofikiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### Twajua maana ya mikataba?

Na Barnabas Maro

**MAANA** ya mkataba ni makubaliano yanayofanywa kwa maandishi baina ya watu, nchi au kampuni moja ama zaidi kwa ajili ya jambo fulani. Makubaliano rasmi ya maandishi baina ya pande mbili.

Tuangalie usajili wa wachezaji wa kandanda, hasa kwa vilabu vyetu nchini. Je, hufanywa kwa manufaa ya vilabu? Hakuna ujanja unaofanywa na baadhi ya viongozi wenye tamaa ya kujinufaisha, wasiojali vilabu vyao?

Kwa upande mwingine, hakuna ulaghai (tabia ya udanganyifu wa kutumia maneno; utapeli) unaofanywa na viongozi waroho wanaogombea uongozi ili kujinufaisha? Viongozi wa aina hiyo wana lugha yao iitwayo 'kupiga pesa/hela!'

Maana yake baadhi ya viongozi kuwasiliana na kushirikiana na wachezaji wanaotakiwa na vilabu vyao kwa kuwaambia waongeze kiasi fulani cha hela ili ziada wachukue wao!

"Fedha fedheha." Fedha huweza kuleta mambo ya aibu baina ya binadamu. Methali hii hutumiwa kutuonya kuhusu maovu yanayoweza kusababishwa na fedha. Viongozi wenye tabia hiyo hutafuta wachezaji ili nao waambulie kile kisemwacho 'kidogo kitu!'

Kwa kawaida, wachezaji wanaotakiwa hufuatiliwa namna ya uchezaji wao kwa muda usiopungua mwaka mmoja au zaidi. Kadhalika ufuatiliaji huo unahusu tabia na nidhamu ya wachezaji wakiwa wanapokuwa nje na ndani ya uwanja. Sasa tuje kwenye suala la Yanga na mchezaji Mghana aitwaye Bernard Morrison aliyesajiliwa msimu huu unaokaribia kufikia tamati. 'Tabia' ni mazoea yanayotokana na mtu kufanya jambo kwa kulirudiarudia hasa baada ya kujifunza au kuiga; mwenendo. 'Nidhamu' ni mpangilio maalumu wa kufanya jambo; adabu ya mtu mbele ya wengine. Tabia nzuri inayolingana na maadili; staha na heshima.

Wahenga wametuachia methali isemayo: "Tabia ni kia (kiungo) cha mwili." Maana yake tabia ni kama kiungo cha mwili. Methali hii hutumiwa kupigia mfano tabia ya mtu ambayo haiwezi kubadilika hata kama watu watafanya jambo la aina gani. Nathubutu kusema Morrison ameonesha udhaifu wake.

Kwanza sifa inamfanya awe na kiburi; pili hana nidhamu na tatu anapotezwa na tamaa ya hela. Ni wazi kuwa hakuna asiye na tamaa ya hela lakini akumbuke kuwa tamaa mbele mauti nyuma chambilecho (kama walivyosema) wahenga.

Kiburi: Tangu alipoonyesha staili (mtindo) yake ya kutembea juu ya mpira uwanjani na jezi yake kununuliwa kwa wingi kuliko jezi ya mchezaji yeyote, amejifanya bora kuliko wachezaji wote wa Yanga!

Pili: Hana nidhamu. Kwa kulewa sifa, anafanya mambo ya kushangaza ikiwamo kukataa kutii kanuni za usajili wake na Yanga. Anaweza kuamua kutokwenda mazoezini akidai kuumwa na hivyo kutocheza mechi.

Hivi karibuni alikataa kusafiri na wachezaji wenzake kwenda Shinyanga na Dodoma. Hata alipotakiwa kuungana na wenzie kwenye mechi dhidi ya Namungo hakuonekana!

Mbaya zaidi alitoroka wakati wenzake wakiwa kambini na kuna madai kuwa alipokuwa akipanda basi, alizuiwa na mlinzi wa kambi lakini akamtishia kwa kisu kisha akaondoka!

Ingawa Morrison alikana kutia saini mkataba mpya, Yanga wanasema mkataba wake na klabu hiyo upo TFF kwa ushahidi. Viongozi wa shirikisho hilo hawajasema lolote kuhusu 'vuta nikuvute' kati ya Yanga na Morrison. Kwa nini?

Viongozi, wanachama na mashabiki wa Yanga wanapaswa kutambua hakuna mchezaji yeyote anayeweza kuitikisa Yanga hata kama atazifunga timu pinzani kwa kufunga magoli kwa kuuamuru mpira uingie golini kwa macho (ingawa jambo hilo haliwezekani).

Vilevile tangu Yanga ilipoanzishwa mwaka 1935 imekuwa na wachezaji wengi wenye sifa mbalimbali. Walikuwepo na wametoka; ama wamezeeka au kufariki lakini klabu ipo pale pale. Kadhalika Morrison anapaswa kufahamu kuwa anapokuwa kiwanjani hachezi peke yake dhidi ya timu pinzani bali huwa na wenzake tisa wanaopambana huku nyuma mlinda mlango akilinda lango lake.

Bila msaada wa wenzake, Morrison asidhani anaweza kufanya lolote uwanjani dhidi ya timu pinzani. Lazima atambue kuwa kabumbu ni wachezaji 11 kila upande na ili timu ishinde, lazima wachezaji washirikiane.

Kwa hiyo ushauri wangu kwa Yanga ni huu: Morrison ailipe klabu kwa kuvunja mkataba. Muhimu zaidi Yanga wawe na utamaduni wa kuwachunguza wachezaji wanaotaka kuwaajiri hata kama watauchezea mpira kwa ulimi kama mtindo huo unawezekana na kukubalika.

Viongozi wasikurupuke kumsajili mchezaji yeyote ndani na nje ya nchi kwa sifa za kulijua sana kandanda bila kufanya utafiti wa tabia zake ndani na nje ya uwanja, ushirikiano na wachezaji wenzake na heshima kwa viongozi.

Yanga imwache Morrison aende atakako na Yanga itabaki kuwa Yanga bila yeye kama alivyoikuta.

**Marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# BURIANI RAPHAEL MCHAMBI KIBIRITI



Baba mzazi wa aliyekuwa mmoja wa wahariri wa siasa wa gazeti la Nipashe linalochapishwa na kampuni ya The Guardian Ltd, marehemu Raphael Mchambi Kibiriti, wakati wa misa ya kuuaga mwili wake katika Kanisha Katoliki Wazo jijini Dar es Salaam jana, na baadaye kuzikwa katika makaburi ya Wazo. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**




Mke wa marehemu Kibiriti, Lilian, akilia kwa uchungu wakati wa kuuaga mwili wa mume wake.



Watoto wa marehemu, Rodgers na Louis, wakiongoza kutoka kanisani baada ya misa.



Waombolezaji wakiaga mwili wa marehemu.



Wafanyakazi wenzake marehemu Kibiriti, wakitoa heshima zao za mwisho.



Mwili wa marehemu, ukiingizwa kaburini kwa mazishi.

# Kambi ya corona Pwani yafungwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amefunga kambi ya wagonjwa wa corona iliyokuwa Lulanzi, Kibaha mkoani Pwani.

Akifunga kambi hiyo jana , alisema hadi sasa zimebaki kambi 11 kati ya 85 zilizokuwa zinahudumia wagonjwa wa corona ambazo nazo zinaendelea kufungwa kutokana na ugonjwa huo kuendelea kutokomea nchini.

Hata hivyo, aliwasihi wananchi kuacha kubweteka na badala yake kuendelea kuchukua tahadhari ya ugonjwa huo katika maeneo mbalimbali ili kuepuka kupata maambukizi mapya.

"Tumefunga kambi 74 hadi sasa na hii hapa Lulanzi ilikuwa kati ya kambi kubwa ambayo ilikuwa inapokea wagonjwa wengi na leo (jana) naifunga rasmi kwani mgonjwa wa mwisho hapa aliruhusiwa Mei 26. Hakuna mwingine aliyepokelewa hadi leo (jana)," alisema.

Waziri Ummy pia aliwataka wakazi wa Kibaha kufika katika Hospitali ya Wilaya kupata huduma na kuondoa hofu ya kuwa kituoni hapo bado kuna wagonjwa wa corona.

Alisema wananchi wanatakiwa kuondoa hofu kwani majengo yote yamefanyiwa usafi baada ya wagonjwa kuondoka katika hospitali. "Lulanzi si tena kambi ya wagonjwa wa corona. Wananchi ondoeni wasiwasi na mfike kupata huduma za afya. Tusikimbilie Tumbi, ile ni hospitali ya rufaa (rufani), tungependa ibaki kutoa huduma za hadhi ya rufaa," alisema Ummy.

Alitumia nafasi hiyo pia kutoa wito kwa Halmashauri ya Mji wa Kibaha kusimamia utoaji wa huduma za viwango vinavyostahili kwa wagonjwa.

Naye Mbunge wa Kibaha Mjini, Sylvestry Koka, alimshukuru Rais John Magufuli kwa hospitali hiyo ambayo imemaliza uhitaji wa hospitali ya wilaya aliyokuwa akiomba kwa zaidi ya miaka saba iliyopita.

Koka aliwataka wananchi kufika kutibiwa katika Hospitali hiyo ambayo imeondoa kilio cha uwapo wa hospitali ya wilaya.

Alisema changamoto iliyopo katika hospitali hiyo kwa sasa ni ubovu wa barabara na gari la wagonjwa ambalo Waziri Ummy aliahidi litapatikana hivi karibuni.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Dk. Tulitweni Mwinuka, alisema hospitali hiyo imeanza kutoa huduma za kawaida kwa wagonjwa Juni 6, mwaka huu, na kwamba jamii bado ina wasiwasi wa kufika katika hospitali hiyo.




Meneja wa Mawasiliano wa Tigo Tanzania, Woinde Shisael, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kampuni hiyo, kuwa mdhamini rasmi wa mawasiliano katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa kwa mwaka wa tano mfululizo. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Theresa Chilambo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lukuvi ageukia vijiji vya mwelekeo wa miji

**Na Munir Shemweta,** KIGOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amewataka maofisa mipango miji kuhakikisha maeneo yote ya vijiji yanayochipukia kuwa miji anapelekewa ili ayatangaze kuwa maeneo ya mipango miji.

Lukuvi alisema hayo juzi wakati akizindua ofisi ya ardhi mkoa wa Kigoma ikiwa ni mfululizo wa uzinduzi wa ofisi za ardhi katika mikoa mbalimbali nchini. Tayari ofisi za ardhi kwenye mikoa ya Tanga, Arusha, Manyara, Singida, Iringa, Njombe, Songwe, Rukwa, Katavi zimezinduliwa.

Alisema wizara yake kwa sasa ina mpango wa kupima kila kipande cha ardhi nchi nzima sambamba na kuhakikisha maeneo yanapangwa ili kuepuka ujenzi holela. "Maeneo yote ambayo vijiji vinachipukia nileteeni nitangaze kuwa maeneo ya mipango miji na maofisa mipango miji mzisaidie wilaya katika hili," alisema Lukuvi

Kwa mujibu wa Waziri Lukuvi, baada ya maeneo hayo ya vijiji vinavyochipukia kutangazwa maeneo ya mipango miji wananchi wake hawatapewa tena hati za kimila na badala yake watapata hati za miaka 99 kama wanavyopata watu wanaoishi mijini.

Alisema mpango wa kuyatangaza maeneo hayo si lazima uanzie wizarani bali maofisa mipango miji katika halmashauri za wilaya wanatakiwa kuyawahi ili kuepuka ujenzi holela.

Kuhusu utendaji kazi katika ofisi za ardhi za mikoa, Lukuvi alisema ofisi hizo zimekamilikia kutokana na kuwa na wataalamu wa fani zote kama vile upimaji, uthamini, mipango miji na usajili wa hati na kubainisha kuwa vifaa vya kisasa vya upimaji navyo vimepelekwa kwenye ofisi hizo.

Kutokana na hali hiyo, alisema kwa sasa mwananchi halazimiki kufika wizarani kwa kuwa huduma zote zinapatikana ofisi za mikoa.

Kuhusu upungufu wa watumishi wa sekta ya ardhi kwenye halmashauri za wilaya, Lukuvi alisema kuwa baada ya kupeleka watumishi ngazi ya mkoa, kazi inayofuata ni kuwapanga upya watumishi katika ngazi ya halmashauri kwa kuzingatia wataalam wa fani zote.

Katika hatua nyingine, Lukuvi ameagiza wananchi wote waliopimiwa ardhi kwenye mkoa wa Kigoma kwenda ofisi za halmashauri za wilaya kuomba kutengenezewa hati na kubainisha kuwa atakayeshindwa baada ya siku 90 atapelekewa hati ya malipo na kudaiwa kuanzia tarehe aliyopimiwa kiwanja chake.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Kigoma, Chediel Mrutu, alisema mkoa huo una wamiliki wa viwanja 14,746 ambao hawajachukua hati pamoja na kukamilika taratibu zote za umilikishwaji ikiwamo kuwekewa alama.

Alisema hatua hiyo inaikosesha serikali mapato sambamba na wamiliki wake kukosa fursa za kiuchumi zinazotokana na kuwa na hati miliki.

## BRELA yajivunia kuondoa urasimu

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA), umejivunia kuondoa urasimu kwenye upatikanaji wa leseni hali ambayo imeondoa malalamiko yaliyokuwapo awali na watu sasa wamekuwa wakipata leseni kwa wakati.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Godfrey Nyaisa, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara, yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Nyaisa alisema hivi sasa wameweka mazingira mazuri na hakuna mfanyakazi anayeweza kuzembea na kusababisha usumbufu kwa mteja hivyo amewakaribisha wanaotaka kusajili biashara mpya na kampuni kujitokeza kwa wingi.

"Tumeamua kuwatumikia Watanzania kwa dhati kabisa na kwetu pale tukigundua mtumishi wetu wamefanya jambo baya kwa mteja hakuna cha nini wala nini tunamuondoa kwasababu tumeamua kufanyakazi," alisisitiza Nyaisa.

Aidha, alisema wameweka vijana mahiri ambao wamekuwa wakiingia kwenye mitandao na kuchukua hoja za wananchi mbalimbali na kuziwasilisha kwa wataalamu ambao huzijibu.

Alisema hali hiyo ndiyo imeondoa misururu ya wananchi waliokuwa wakijazana kwenye ofisi za taasisi hiyo kwaajili ya kupata majibu ya maswali mbalimbali waliyokuwa nayo wakati huo. "Brela tunawategemea sana wateja wetu, ndiyo maana hatutaki urasimu wala rushwa kabisa watu waje hata huku sabasaba watapata majibu ya hoja zote walizonazo maana timu nzima iko huku kwaajili ya kuwasikiliza," alisema Nyaisa

Alisema miongoni mwa maboresho waliyoyafanya ni kuhakikisha shughuli zote zinafanyika kwa njia ya mtandao ili wananchi wasipate usumbufu wa kwenda kwenye ofisi hizo kupanga foleni kwaajili ya kusubiri huduma zao.

Alisema wameweka mifumo ya utendaji kazi ambapo mtumishi wa Brela halazimiki kukutana na mteja kwani anaweza kujisajili kwa njia ya mtandao popote alipo na kupata cheti cha usajili kwa mtandao.





Ofisa Afya Mazingira kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nashri Mahiki (kushoto), akizungumza na viongozi vya vyama vya watu wenye ulemavu (SHIVYAWATA) na waandishi wa habari, wakati wa mafunzo ya elimu jumuishi ya namna ya kuchukua tahadhari juu ya maambukizi ya ugonjwa wa corona, yaliyoandaliwa na kanisa la FPCT, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wizara yajipanga kwa corona uchaguzi mkuu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imejipanga kuhakikisha vyama vya siasa vinazingatia miongozo ya kujilinda dhidi ya maambukizi ya corona wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Ofisa Afya na Mazingira wa wizara hiyo, Nashri Mahiki, aliyasema hayo jana alipozungumza na viongozi vya vyama vya watu wenye ulemavu (Shivyawata) jijini hapa.

Walikuwa wakenye mafunzo yaliyoandaliwa na Kanisa la FPCT Dodoma kuhusu kudhibiti maambukizo ya ugonjwa huo katika mikusanyiko ya watu.

Mahiki alisema wizara imejipanga kuhakikisha kwenye mikusanyiko hiyo ya kampeni, elimu inatolewa kwa watu wote ili kujikinga na maambukizi hayo.

"Hatua zote zilizochukuliwa na kuufanya ugonjwa huu kupungua kabisa ndiyo hizo hizo zitakazotumika kwa kutoa elimu zaidi juu ya kujilinda, ili kampeni hizo zifanyike kwa tahadhari na usalama kwa watu watakaokusanyika," alisema.

Alisema elimu ya kujikinga imekuwa ikitolewa ili kufikia makundi yote, wakiwamo watu wenye ulemavu.

Aliwataka waandishi wa habari na viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu kuwa mabalozi kwa kuendelea kutoa elimu hiyo ya kujilinda dhidi ya maambukizi ya ugonjwa huo.

Ofisa Mradi wa Elimu Jumuishi wa Kanisa la FPCT wilaya ya Dodoma na Bahi, Jane Mgidange, alisema mafunzo hayo yamefanyika ili kuyapa elimu makundi maalum ya watu wenye ulemavu, wafahamu na kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Alisisitiza kufuatwa kwa miongozo iliyotolewa na wizara hiyo ili kutokomeza ugonjwa huo nchini.

# Uzalishaji wa kuku kuongezeka nchini

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imejipanga kuongeza uzalishaji wa kuku kupitia vikundi vya vijana, ili kujikwamua kiuchumi na kukidhi mahitaji ya soko nchini.

Mkurungenzi wa Uzalishaji na Masoko wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Felix Nandonde, alibainisha hayo alipokabidhi vifaranga vya kuku 650 wa nyama kwa kikundi cha vijana cha Asacri cha jijini.

Dk. Nandonde alisema wizara imeendelea na utaratibu wa kukabidhi misaada ya vifaranga vya kuku kwa makundi ya vijana, ili kuwakwamua kiuchumi na kutoa ajira kwao.

Alibainisha kuwa msaada huo ni miongoni mwa mikakati ya wizara hiyo ya kuyahamasisha makundi mbalimbali ya kijamii kupenda ufugaji wa kuku.

"Leo tumekabidhi vifaranga vyenye thamani ya Sh. milioni tatu na tunatarajia kuongeza kadri ya bajeti ya wizara itakavyoruhusu, ili kuzalisha kuku wengi kukidhi soko la wakazi wa Jiji la Dodoma,"alisema.

Alisema wizara hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Akm, wametoa idadi hiyo ya vifaranga wa nyama, ili kuongeza nguvu katika ufugaji wa kuku nchini.

Alisema mbali na msaada huo, wamekabidhi vifaa, chakula na dawa kwa ajili kuwahudumia kuku hao na uongozi wa jiji utatoa madaktari kwa ajili ya kuwapa mafunzo namna ya kuwahudumia kuku hao. Alisema mpaka sasa, kuna kuku milioni 79.1 nchini. Kati yao, wa kienyeji ni milioni 38.5 na wa kisasa milioni 40.6.

Aliongeza kuwa mpango huo wa kuyawezesha makundi ya vijana utakuwa endelevu na unafanyika kwa awamu katika mikoa mbalimbali nchini.

Kijana Abdalah Chavuma kutoka Kikundi cha Asacri, alisema kikundi chao kinaundwa na vijana 10 wa jinsia tofauti ambao ni wahitimu wa vyuo vikuu mbalimbali nchini.

Chavuma alisema kikundi chao kinajihusisha na ufugaji wa kuku, sungura na bata na wako katika maeneo ya Nkuhungu na Chidachi jijini hapa.

Meya wa Jiji la Dodoma, Profesa David Mwamfupe, alisema moja ya malengo ya jiji hilo ni kuhakikisha wanayawezesha makundi mbalimbali ya kiuchumi.

Profesa Mwamfupe alisema mbali na uongozi wa jiji kutoa fedha kwa ajili ya makundi hayo, pia wanawezeshwa mikopo ya ng'ombe wa maziwa, ili kujiajiri na kuajiri wengine.

Profesa Mwamfupe aliyataka makundi hayo ya vijana kuchangamkia fursa za ajira zinazojitokeza katika maeneo yao.

# Usafirishaji dhahabu ghafi mbioni kuzuiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Madini, Profesa Simon Msanjila, amesema serikali itasitisha usafirishaji wa dhahabu ghafi kwenda nje ya nchi kusafishwa baada ya viwanda vya usafishaji madini hayo kuanza kazi nchini.

Profesa Msanjila alitoa kauli hiyo jana alipofanya ziara ya kikazi katika Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu (Refinery) cha Eyes of Africa Ltd kilichoko Area D pembezoni mwa Uwanja wa Ndege wa Dodoma.

Alisema mara baada ya viwanda vya usafishaji madini ya dhahabu kuanza kazi, serikali itasitisha usafirishaji wa dhahabu ghafi kwenda kusafishwa nje ya nchi na badala yake madini ghafi yote yatasafishiwa nchini kabla hayajasafirishwa kwenda nje ya nchi.

"Lengo la ziara hii ni kukagua hatua za ujenzi uliofikiwa na kiwanda hiki ambacho ni kiwanda cha kwanza nchini cha kusafisha madini ya dhahabu na fedha," alisema.


Alisema kiwanda hicho ni miongoni mwa viwanda vya kampuni nne zilizopewa leseni ya usafishaji wa madini ya dhahabu (Gold Refinery Licence) nchini. Kampuni nyingine ni Stamico-Mwanza, Geita Gold Refinery na African Ayes-Geita.

Katika ukaguzi huo, Profesa Msanjila alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Eye of Africa, Ferenc Molnar, kuandika barua kwa serikali kupitia Wizara ya Madini, akiainisha mambo muhimu yanayotakiwa, ili serikali isaidie katika kufanikisha mahitaji ya kampuni hiyo.

Profesa Msanjila pia aliahidi kampuni hiyo kuwa serikali itahakikisha inapata wateja kutoka sehemu mbalimbali hususan wachimbaji wadogo mara itakapoanza uzalishaji.

Alimpongeza Molnar kwa hatua nzuri aliyoifikia ikiwamo ufungwaji wa mashine mbalimbali za kusafisha madini ya dhahabu katika kiwanda hicho.

Mkurugenzi Mtendaji huyo alisema kuwa mara baada ya kuanza kwa uzalishaji, kampuni yake itakuwa na uwezo wa kuzalisha kilo 40 za dhahabu kwa siku na itamtoza mteja asilimia 0.5 ya gharama ya mzigo utakaosafishwa kiwandani hapo.





Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Maendeleo ya Wazee, Wanawake na Watoto Zanzibar, Moudline Castiko (kulia), akizumgumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, kuhusu maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tamwa yawapa mafunzo walionyanyasika kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kimewapa mafunzo ya ufugaji wa kuku wanawake 10 walioathirika kwa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo kutelekezwa kisiwani Pemba.

Mafunzo hayo yaliyojumuisha waathirika wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kutoka Wilaya za Wete na Mkoani Pemba, yamelenga kuwawezesha wanawake kujiendeleza kiuchumi baada ya kukumbana na udhalilishaji huo.

Mratibu wa chama hicho Ofisi ya Pemba, Fat-hiya Mussa Said, alisema jana kuwa lengo la kutolewa kwa mafunzo hayo ni kuwawezesha wanawake kujisimamia kiuchumi baada ya kukumbwa na udhalilishaji ikiwamo kutelekezwa.

"Tumebaini kwamba sababu kubwa ya kuwapo kwa wimbi la ubakaji na udhalilishaji katika jamii ni mifarakano ya kifamilia na utelekezaji, hivyo TAMWA Zanzibar imeamua kuandaa mafunzo haya ili yawasaidie waathirika wa vitendo hivyo kujishughulisha katika shughuli mbalimbali za kiuchumi," alisema.

Mwezeshaji wa Mafunzo hayo, Omar Hamad Mjaka, alisema yamejikita katika kuwapatia mbinu mpya za ufugaji wa kisasa, ili uwasaidie kuimarisha vipato vyao na kujikimu kiuchumi.

"Mafunzo haya yanalenga kuwapatia elimu na mbinu mpya za ufugaji wa kuku kwa kutumia njia bora za kisasa na kuondokana na ufugaji wa mazoea kwa lengo la kukuza uchumi wa familia," alisema. Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Riziki Said Khatib, aliishukuru TAMWA Zanzibar kwa kuwezesha mafunzo hayo, akiamini yatawasaidia kujikwamua kiuchumi kutokana na hali ngumu ya maisha wanayokabiliana nayo.

"Tunashukuru sana kwa mafunzo haya, tunaamini kupitia ufugaji itatuwezesha kujisimamia wenyewe na kuendesha familia zetu ikiwa ni pamoja na kuwasomesha watoto wetu," alisifu.

Utoaji wa mafunzo hayo kwa Wanawake ni utekelezaji wa mradi wa Jukwaa la Wanahabari la kumaliza vitendo vya udhalilishaji Zanzibar unaotekelezwa na TAMWA Zanzibar kwa ufadhili wa Danish International Development Agency (DANIDA).

# ZHC yampa miezi 6 mjane wa jaji kukabidhi nyumba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Nyumba la Zanzibar (ZHC ), limemtaka mjane wa marehemu Jaji Mkusa Issac Sepetu, kuhama na kukabidhi nyumba ya shirika miezi sita tangu kufariki kwa mumewe Febuari 16 mwaka huu.

Agizo hilo limetolewa na Mkurugenzi wa Shirika hilo, Riziki Jecha Salim, kupitia barua aliyotumiwa mke wa marehemu, Salma Mkusa, kwa madai nyumba hiyo ilikuwa ikitumika kinyume cha masharti ya ukodishwaji.

Kwa mujibu wa barua iliyotolewa na mkurugenzi huyo Juni 24, mwaka huu, yenye kumbukumbu namba ZHC/HNO.9/116/11, Salma anatakiwa kuondoa mali za marehemu na kukabidhi funguo.

Katika barua hiyo ambayo Nipashe imeiona, imeonywa kuwa iwapo mjane huyo atashindwa kutekeleza amri hiyo, shirika litachukua hatua ya kuhamisha mali zilizomo ndani ya nyumba na kuzihifadhi kwa gharama zake (mjane).

Nakala ya barua hiyo pia imetumwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, Mrajisi Mahakama Kuu, Polisi Kituo cha Mwembe Madema na Sheha wa Shehiya ya Miembeni na kutakiwa zoezi hilo kutekelezwa Jumatatu ijayo.

Kwa mujibu wa barua hiyo, sababu za mjane kutakiwa kurejesha nyumba kuwa ni mtoto wa kufikia wa marehemu Jaji Mkussa, amekuwa akifika katika nyumba hiyo namba 9/116 iliyoko katika magorofa ya Michenzani anapokwenda kumsalimia mama yake na ndugu zake wakati anaishi Uingereza.

"Nyumba namba 9/116 Michenzani alimpa mwanaye anaeishi Uingereza na shirika lina taarifa rasmi nyumba hiyo haishi mtu na imefungwa kwa muda mrefu." inaelezwa katika barua hiyo.

Salma aliwaambia waandishi wa habari nyumbani kwake Michenzani jana kuwa, alianza kutakiwa kuhama katika nyumba hiyo akiwa bado kizuka na kupewa siku saba kuondoka ndani ya nyumba hiyo.

"Sijawahi kuona mpangaji yeyote anafukuzwa ndani ya nyumba kwa muda wa siku saba katika maisha yangu, lakini nilipeleka ombi la kuwa mpangishwaji baada ya mume wangu kufariki bila kujibiwa na kuanza kufukuzwa," alilalamika.

Salma alisema kuwa kwa mujibu wa mkataba uliofikiwa kati ya shirika na marehemu ulioti-

# Waziri ataja kiini cha udhalilishaji Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kazi, Uwezeshaji Wanawake, Watoto na Wazee, Mauldline Castico, amesema matukio ya udhalilishaji wa kijinsia yamekuwa yakiendelea Zanzibar kutokana na jamii kukataa kutoa ushahidi mahakamani.

Castico alisema hayo juzi wakati akikabidhi tuzo kwa waandishi wa habari ambao walishiriki katika mradi wa kuandika habari za matatizo yanayowakabili wanawake na watoto katika kupata haki zao msingi.

Alisema wapo baadhi ya wananchi hawatoi ushirikiano katika kuzipatia ufumbuzi kesi za udhalilishaji wa kijinsia na matokeo yake ni kufutwa kwa kesi hizo mahakamani.

"Tunazo sheria nzuri za haki ya watoto pamoja na kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, lakini tunakabiliwa na 'muhali' ikiwamo kukataa kutoa ushahidi mahakamani," alisema.

Aliwataka waandishi wa habari kuendelea na kuvipatia ufumbuzi vikwazo mbalimbali vinavyowakabili wanawake na watoto ambavyo ni tatizo katika kuyafikiya maendeleo kwa makundi hayo ikiwamo sekta ya elimu.

"Waandishi wa habari fanyeni kazi ya kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili wanawake na watoto, tutatoa ushirikiano wa dhati katika suala hilo," aliahidi.

Katibu wa Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo (WAHAMAZA), Salma Said, alisema mafanikio makubwa yamepatikana katika mradi wa kuandika habari za maendeleo vijijini kwa ajili ya kufichua matukio ya udhalilishaji kwa watoto na kuona wanapata haki zao za msingi.

"Matatizo yanayowakabili watoto ni mengi, juhudi zaidi zinahitajika kuona kwamba watoto wanaondokana na matatizo na changamoto ambazo ni kikwazo katika kuyafikiya malengo ikiwamo elimu," alisema.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF) anayeshughulikia miradi, Maha Damaj, aliwataka waandishi wa habari kuendelea kutekeleza majukumu yao na kufanya uchunguzi wa matukio ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ambavyo hurudisha nyuma maendeleo ya watoto na ukuaji wao kwa ujumla.

"Bado hatujafanikiwa kukomesha vitendo vya udhalilishaji kwa watoto, ninawaomba waandishi wa habari waliopata mafunzo hayo, kuendelea kuvifuatilia vikwazo vinavyokwamisha watoto kupiga hatua kubwa ya maendeleo," alisema. Waandishi wa habari 15 walishiriki katika mradi wa kuandika habari mbalimbali zinazohusu ukatili wa kijinsia kwa watoto ambapo miongoni mwa matatizo makubwa waliyobaini kwa watoto ni ukosefu wa vyeti vya kuzaliwa na kuwapa wakati mgumu wazazi wakati watoto wao wanapoanza elimu ya msingi katika usajili wa kuanza shule.



**KANYE WEST, KIM WAUMBULIWA** Uk.14

JUMAMOSI JULAI 4, 2020

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# ZUCHU NI BRENDA FASSIE MPYA?

MSANII wa kike wa muziki wa Bongo Fleva, Zuchu, anaendelea kuonyesha kipaji chake na kumfanya kuwa tishio kwa wasanii wengine ambao wamelishika soko.

Ikumbukwe, tangu atambulishwe na lebo yake, Zuchu, amekuwa akidondosha ngoma zake kila kukicha, na kila ikitoka inakuwa tamu zaidi ya ile ya awali.

Katika kipindi hiki ambacho Tanzania inaingia kwenye uchaguzi mkuu, Zuchu anaonekana kuwapiku wasanii mbalimbali waliojitokeza kutunga nyimbo kwa ajili ya kunogesha kampeni za vyama vya siasa hasa CCM.

Ngoma yake mpya inayoitwa 'Tanzania ya Sasa' imekuwa gumzo kutokana na kupendwa na kila kiongozi na mwanachama wa CCM.

Katika kile kinachoonekana imewanogesha vilivyo, hivi karibuni alionekana Rais Dk. John Magufuli na wajumbe wa kamati kuu ya CCM, wakiserebuka na kibao hicho kabla ya kuanza kwa kikao.

Kama wimbo wake itakuwa namba moja katika kampeni za CCM, basi msanii huyo atafuata nyayo za Brenda Fassie, ambaye kibao chake cha 'Vulindlela' kinatumiwa na chama cha ANC kama wimbo wake maalum ndani ya chama.

Brenda ambaye alifariki mwaka 2004, alikuwa msanii pekee wa kike ambaye chama cha ANC, kilimtumia kama alama ya ushindi.

Kutokana na wimbo wa 'Tanzania ya Sasa' kuonekana kuwa wa kimapinduzi zaidi, Zuchu anaweza kutumia mwanya huo kuongeza umaarufu wake na kuwa Benda Fassie mpya.

BASI SAWA

## Baba Levo sasa fuata uzazi wa mpango

MKONGWE wa muziki wa Bongofleva na Diwani wa Mwanga Kaskazini, mkoani Kigoma, Baba Levo, amesema ana watoto wengi hadi wengine amewakataa kwa sababu mama zao walikuwa hawajatulia.



Akizungumza na Planet Bongo ya East Africa Radio, Baba Levo amesema yeye ni baba bora kwa watoto wake, tatizo kutokana na wingi wa watoto alionao anahitaji vipimo vya DNA ili kuthibitisha.

"Napenda sana watoto japokuwa nina watoto wengi, lakini wengine nimewaweka pembeni kwa sababu wakati natafuta hiyo mimba mama zao walikuwa hawajutulia, walikuwa wana rukaruka, leo katembea na huyu kesho katembea na yule, halafu akipata mimba anakwambia ya kwako," amesema.

## Gabo ulitaka ustaa mwenyewe, sasa usilie

MWIGIZAJI wa BongoMuvi, Gabo Zigamba, amewataka watu kuacha kuzungumzia suala la yeye kuoa kwa siri, kwa sababu mambo yake binafsi hapendi watu wengine kujua.

Taarifa za msanii huyo wa filamu kuoa zilikuja baada kusambaa kwa picha mitandaoni mwezi wa Aprili, zikimuonyesha katika mavazi na mazingira yaliyoashiria kafunga ndoa.




"Huwa sipendi kuzungumzia hivyo vitu kwa sababu kuna vitu viwili, kwanza mtu anayeniona anatafuta uhamasishaji kutoka kwangu, sasa kuhusu ndoa siwezi kumhimiza mtu na haifanani kabisa sawa na duka la vipodozi kwenda kuulizia sigara".

"Pili Suala la mimi kuoa au kutokuoa kwa mtu ambaye anamfuatilia Gabo Zigamba haimsaidii chochote, kuoa, kuolewa au kufanya maulid haina uzito wowote kwa jamii, hayo ni mambo ya mtu binafsi japo Ulaya wanafanya sana hizo Style kwa sisi bado hasa ukiangalia soko letu halipo rasmi, kuna vitu vingi vya kupiga kelele ili tuweze kusogea" ameongeza.



# Rostam wakumbuka wagonjwa

WANAMUZIKI wanaounda kundi la HipHop la Rostam, Roma na Stamina, wamefanikiwa kutoa msaada katika hospitali mbili kutokana na pesa zilizopatikana kupitia kibao chao cha 'Kaka Tuchati'.

Msaada waliotoa ni pamoja na mashine mbili za kusaidia wagonjwa kupumua na shuka 68.

Vifaa hivyo vimenufaisha hospitali za mkoa wa Tanga na Morogoro.

# Mchumba: Haimo, haimo basi huwa

**Na Adam Fungamwango**

WASWAHILI wana msemo wao mmoja kuwa 'mzaha mzaha, hugeuka usaha'. Maana ya msemo huu ni kwamba kitu chochote kiwe kizuri au kibaya, kikiwa na mazoea hugeuka kuwa tabia, utamaduni au sheria.

Kwenye jamii mambo haya yanatokea sana, unaweza kutoa hata msaada tu, baadaye ikaonekana ni kanuni na usipotoa, unaonekana mbaya. Huu ni mfano tu.

Kwenye filamu hii inayoitwa 'Mchumba' kuna kitu kilijitokeza, lakini ikaleta athari miaka mingi iliyofuata.

Filamu hii imechezwa na wasanii Abdallah Mohamed, Jenipha Temu, Kipupwe, na wengineo wengi.

Kipupwe ambaye alicheza kama Nyembo, baada ya kukaa na mkewe Ndindi kwa muda mrefu jijini Dar es Salaam waliamua kuhamishia maisha yao kijijini.

Huko wanaanza maisha mapya, lakini kuna kitu kinajitokeza. Kuna mwanadada mmoja Siwazuri anajitokeza na kumwambia Nyembo kuwa anampenda na anatamani amuoe. Nyembo anamwambia hawezi kumuoa kwa sababu ana mke mwingine.

Hata hivyo, Siwazuri hasikii wala haambiwi, waziwazi anataka aolewe na Nyembo na akafikia wakati akaenda hadi nyumbani kwake mbele ya mkewe.

Ndindi, mke wa Nyembo anaonekana kushangazwa na tukio hilo na kumtimua msichana huyo Siwazuri.

Kuna kijana mmoja wa kitajiri anajitokeza kutaka kumuona Siwazuri, lakini msichana huyo anakataa katakata na kudai kuwa yeye anataka kuolewa na Nyembo.

Habari zinatapakaa kijijini, ikabidi mke wa Nyembo, akamkalisha mumewe kitako kutaka kujua ni kitu gani hasa kilichomfanya msichana yule kumng'ang'ania kiasi cha kuhatarisha hata maisha yake?

Kumbe miaka mingi iliyopita Siwazuri alifiwa na wazazi wake wote, akiwa na miaka mitano tu. Akawa analelewa na ndugu. Mtu mmoja ambaye alimzoea zaidi ni Nyembo. Ni kwa sababu alikuwa akimnunulia pipi, buskuti, maandazi kila anapolia kuwakumbuka wazazi wake. Kibaya au kizuri akawa anamwita mchumba. Hiyo ilikaa kichwani mwa Siwa, kiasi chata Nyembo alipoamua kwenda mjini kutafuta maisha, alikuwa akirejea kijijini anamletea nguo, viatu na zawadi mbalimbali.

Haya yote Nyembo alikuwa akifanya mzaha wa kumwita mchumba, alipokuwa akimletea zawadi binti huyo yatima.

Wakati huo Siwa alikuwa taratibu anakua msichana. Alipokuwa Mwari, kwenye akili yake, hakuna mwanaume aliyempenda moyoni mwake kwa dhati kama Nyembo. Ni kwa sababu ya zawadi zake miaka yote, huku akiitwa mchumba.

Mwisho wa siku, baada ya kuona haiwekani kuolewa, Siwa anakunywa sumu na kukimbizwa hospitalini haraka.

Baada ya kuponea chupuchupu, Ndindi mke wa Nyembo anamwita nyumbani na kufanya mazungumzo ya kina.





# Duh! Timbulo kumbe mtoto wa 46

MSANII wa muziki wa BongoFleva,Timbulo, amesema baba yake anamchukulia kama babu yake kutokana na kuwa wengi.

Timbulo amesema kwao walizaliwa jumla ya watoto 46, kwa mama tofauti, huku kwa upande wa mama yake yeye ni mtoto wa mwisho kati ya 13.

"Baba yangu alikuwa na watoto wengi hadi kuna muda alikuwa anatuchanganya, tulizaliwa 46 kwa wake zake wanne tofauti, mimi mpaka najitambua tulikuwa tupo 34 japo kuna wengine walitangulia mbele za haki, mimi kwa upande wa mama yangu tulizaliwa watoto 13 na mimi ndiyo nilikuwa wa mwisho, mimi naona kama ni mjukuu kwa baba yangu kwa sababu alikuwa amezeeka" ameeleza Timbulo.







# Ngoma konki nusu ya 2020

**Na Adam Fungamwango**

MWAKA 2020 umegawanyika. Tayari ni mwezi wa saba na unaendelea kuyoyoma ili kuumaliza mwaka. Kwenye tasnia ya muziki tumeona baadhi ya ngoma zilizotoka katikati ya mwaka na kubamba kila kona.

Wasanii mbalimbali maarufu na chipukizi waliingia studio na kurekodi ngoma zilizotoka mwezi Juni na kuwaburudisha mashabiki wao.

Zipo nyingi, lakini hizi ni baadhi ya ngoma ambazo zimewachetua mashabiki wengi wa Kibongo.

**HAIJAKAA SAWA-MBOSSO**

Kwa siku za karibuni, Mbosso ni msanii ambaye amekuwa akitoa ngoma mpya karibuni kila mwezi. Lakini pia amekuwa akitoa ngoma ambazo zimekuwa zikizungumzia matatizo ya kijamii hasa kwenye ndoa au mapenzi.

Ni mmoja kati ya wasanii wachache wa bongo fleva ambaye amebadilika sana kwenye aina yake ya uandishi wa mashairi, hadi midundo.

Katikati ya mwaka huu amekuja na ngoma yake mpya aliyoiita 'Haijakaa Sawa'.

Ni ngoma inayomhusu jamaa ambaye mambo yake bado hayajakaa sawa, nadhani mpenzi wake amekuwa akilalamika kuhusu ugumu wa maisha.

Mwanaume anambembeleza na kuwambia hata yeye amechoka kula bamia na mlenda, lakini hana namna, kwa sasa anatafuta na ipo siku watafanikiwa kimaisha. Ngoma hiyo ilitolewa Juni 4.

**SO HOT-ALI KIBA**

Ali Kiba naye kwa sasa hajambo. Kuna baadhi ya mashabiki wake na hata wale ambao wanaompinga, wamekuwa wakimkosoa kuwa hutoa ngoma na kukaa kwa muda mrefu mno, kitu ambacho kinamfanya asiwe mwenye mafanikio zaidi kama wenzake.

Sasa baada ya kutoa 'Dodo' miezi miwili iliyopita, katikati ya mwaka amekuja na ngoma yake nyingine mpya iitwayo 'So Hot' ambayo imewekwa rasmi kwenye mtandao wake wa kijamii Juni 8.

**GWIJI-MWANAFA, FT NYOSHI EL SADAAT, MAUA SAMA**

Kama kuna kitu ambacho mashabiki wengi kimewaacha hoi, ni muungano wa wanamuziki wa hip hop na muziki wa dansi, pamoja na R&B.

Hao ni MwanaFA 'Binamu', akiwa na Nyoshi El Sadaat, na mwanadada Maua Sama. Wameungana kwa pamoja na kuja na aina tamu ya muziki katikati ya mwaka kwenye ngoma inayoitwa 'Gwiji.' Ni ngoma iliyoachiwa Juni 17.

**KISWASWADU-AMBER RUTTY FT DAVIL**

Katikati ya mwaka huu kuna mambo yake, kwani msanii mpamba muziki, Amber Rutty, naye amekuja na ngoma yake mpya ambayo ameiita 'Kiswaswadu.'

Imetoka Juni 21 na kwa muda mfupi tu imeshaanza kuwapagawisha mashabiki wengi, kwani imepigwa kwenye mahadhi ya singeli ambayo inatamba kwa sasa uswahilini.

**WAWAPI-S KIDE FT HARMORAPA**

Mwaka una mambo huu, mwezi Juni kumekuwa na ngoma nyingine matata ya singeli ambayo inayoitwa 'Wawapi'. Ni ngoma iliyotoka Juni 3, ikitolewa na msanii S Kide akimshirikisha mmoja wa wasanii machachari, Harmorapa.

# Kanye West, Kim waumbuliwa



RAPA maarufu nchini Marekani, Kanye West na mkewe Kim Kardashian, wametangaza kuingia katika kundi la watu wenye utajiri wa kupindukia.

Hata hivyo, jarida maarufu linalowatambua watu matajiri duniani Forbes, limekanusha taarifa hizo na kueleza Kim bado hajaingia katika hatua hiyo kutokana na hadi sasa ana utajiri wa dola million 900 pekee.

Wiki hii, Kanye aliandika ujumbe kupitia ukurasa wake wa Twitter, kuwa mkewe anakuwa bilionea mwingine baada ya kuingia mkataba mnono wa biashara.

"Ninajivunia kuwa na mke mzuri Kim Kardashian West, sote tunaingia katika ubilionea. Unaweza kusema ni uwendawazimu, Mungu sasa ametuangazia katika familia yetu, tunaomba baraka katika maisha haya," ilisema sehemu ya ujumbe huo.



## Dk. Dree amtandika talaka mkewe

WIKI hii mashabiki muziki nchini Marekani, wameshtushwa na taarifa za mwanamuziki mkongwe, Dk. Dree na mkewe kuachana baada ya kuishi katika ndoa kwa miaka 24.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Dre na mkewe Nicole walifungua jalada la maombi ya talaka siku ya jumatatu, huku ikielezwa hakuna njia ya kunusuru ndoa hiyo.

Mkongwe huyo wa muziki ana utajiri unaokisiwa wa dola milioni 800 na mkewe huyo walioana mwaka 1996 na kupata watoto wawili Triuce na Truly.

## Khloe,Tristan mambo safi

BAADA ya kuachana kwa muda wa mwaka mmoja, mwanamitindo Khloe Kardashian na mpenzi wake wa zamani Tristan Thompson, hatimaye wamerudiana.

Kulingana na mtandao wa PageSix, wawili hao wameamua kuweka tofauti zao pembeni na kuanza ukurasa mpya wa mapenzi.

"Tristan anafanya kazi kubwa ya kuhakikisha anakuwa baba bora na kurudisha tena mapenzi kwa Khloe," kiliaema chanzo kimoja.





## Weinstein azidi kupata aibu

MKONGWE katika sekta ya filamu za Hollywood, Harvey Weinstein, anazidi kupata aibu baada ya taarifa mpya kubaini aliwashambulia kingono zaidi ya wanawake 100.

Licha ya Weinstein kuendelea kutumikia kifungo cha miaka 25 jela, serikali ya New York, imepanga kutoa kiasi cha dola milioni 19, kwa ajili ya fidia kwa wanawake waliokabiliwa na unyanyasaji huo.

Taarifa hiyo inasema walengwa ni wale waigizaji wa sinema ambao walikabiliwa na mazingira mabaya ya kazi, unyanyasaji wa kijinsia na ubaguzi.

## Dbanj bado abanwa koo

SAKATA la ubakaji linalomkabili mwanamuziki Dbanj, limechukua sura mpya, baada ya Inspekta Mkuu wa Polisi (IGP) wa Nigeria, Mohammed Adamu, kuamuru uchunguzi haraka dhidi ya polisi waliokamata mtu Seyitan Babatayo, ambaye ndiye chanzo cha malalamiko hayo.

IGP huyo alimtaka Inspekta Abraham na timu ya maofisa wa Polisi wote wa Ikeja, kutoka Lagos, kufuatilia maombi ya wakili wa Seyitan, kujua kwa nini alishikiliwa baada ya kuibua kashfa hiyo.

Mawakili wa Babatayo, Ojogena na washirika wake wanadai kwamba polisi walitii agizo la D'Banj la kumshikilia mteja wao kizuizini kwa zaidi ya saa 24.



MAKALA

# IKUNGI KATIKA MAAJABU MAKUU UBORESHAJI WA MIRADI YA ELIMU

## ■Darasa 7 wateleza kuiona sekondari

**Na Elisante John,** SINGIDA

MPANGO wa kuinua ubora wa elimu nchini au Equip -Tanzania, ni mradi unaofadhiliwa na serikali ya Uingereza kupitia shirika lake la misaada (DFID-UKAID), kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 100.

Ni mpango unaowezesha shule za msingi kuunda chombo cha ushirikiano kinachojulikana 'Umoja wa Walimu na Wazazi' (UWW), lengo ni kuimarisha uhusiano baina yao, ili kuinua taaluma na kumfanya mwanafunzi aelewe vyema anayofundishwa.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, mpango unatajwa kutoa mchango mkubwa kitaaluma na inaongeza kasi kila mwaka, kutokana na shule kufanya vyema kwenye mtihani wa kumaliza elimu ya msingi.

Ni hali inayowezesha shule za sekondari kufanya vizuri, kutokana na wengi wanaojiunga, kuandaliwa vyema.

Mratibu wa Equip-T, ambaye pia ni Ofisa Elimu Vifaa na Takwimu, wilaya Ikungi, Imani Maketa, anasema maeneo mengi yamefanyiwa kazi tangu mpango ulipoanza mwaka 2018 na kuwezesha elimu kukua wilayani.

Anataja baadhi ya maeneo, ni ufundishaji kwa walimu, uliowabadili wanafunzi wa darasa la pili na tatu kuelewa vyema utangulizi wa 'KKK'; kusoma, kuandika na kuhesabu.

Maketa anasema, kabla mpango kuanza, ilikuwa kawaida mwanafunzi wa darasa la pili hadi tatu kushindwa kusoma.

Eneo lingine ni ufanisi wa waratibu elimu kata, maofisa elimu wilaya, wajumbe kamati za shule, wazazi na jamii wanaohudumia shule husika na wanafunzi na kuwandaa vyema wanaotarajiwa kuanza shule.

Pia, kuna wajumbe wa kamati za shule waliopatiwa mafunzo kuongeza ufanisi kazini, ili kuwa na mkakati wa pamoja wa wazazi na jamii husika, washiriki katika maendeleo ya shule na imeleta tija kwenye mradi.



Mratibu wa asasi ya Equip Tanzania wilayani Ikungi, Mwalimu Imani Maketa, akifafanua jambo ofisini kwake.



Ofisa Elimu Msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Gidion Kitoboli, akiwa kwenye shughuli zake. **PICHA ZOTE: ELISANTE JOHN.**

### DED

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, anamshukuru Rais Dk. John Magufuli, kwa mapinduzi makubwa kwenye sekta ya elimu, hata thamani ya sekta hiyo inaonekana.

Anasema kupitia 'Equip-T' Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi imenufaika na zaidi ya Sh. bilioni 1.4 tangu programu ilipoanza kutekelezwa wilayani, Septemba 2018.

Kijazi anataja yaliyotekelezwa sasa ni ujenzi wa shule shikizi nne, ukarabati vyumba vya madarasa ya shule za msingi, mafunzo ya wawezeshaji vituo vya utayari, semina ya mafunzo ya jinsia na mafunzo ya ukusanyaji taarifa kwenye mfumo (SIS).

Anatumia fursa kuwahimiza wanafunzi kuhudhuria shule bila kukosa, akisema wamewezeshwa kujengwa vyumba vinane vya madarasa na samani zake, ofisi nne za walimu na matundu 24 ya vyoo.

Pia, kuna maboma sita ya vyumba vya madarasa yamekarabatiwa na kumenunuliwa samani katika shule tatu.

### OFISA ELIMU

Ofisa Elimu wa Shule za Msingi Wilaya ya Ikungi, Gideon Kitoboli, anasema licha ya kuwajengea uwezo wa uongozi maofisa elimu kata na walimu wakuu, Equip-T tangu ianze, imeshanufaisha zaidi ya walimu 650 kuwapa mafunzo, ili kuboresha utendaji darasani.

Pia, anasema kuna jumla ya wawezeshaji 62 waliopata mafunzo ya kufundisha kwenye vituo vya utayari, vinavyowandaa wanafunzi kuingia darasa la kwanza, wamepatiwa mafunzo kuendesha shule hizo.

Wahamasishaji jamii, wawili kila shule walipatiwa mafunzo kusimamia wanafunzi 1,200 waliotoka mbali na makazi, wamenufaika kupata nafasi ya kusoma kwenye shule shikizi nne, jirani na makazi yao.

"Kwa kweli naweza kusema mpango huu ni mzuri sana, umenufaisha watoto 3,528 waliokuwa hawawezi kwenda shule za awali kutokana na umbali, lakini waliandaliwa vituo 74 vya utayari vilivyopo maeneo mbalimbali ya wilaya yetu, na kusoma vizuri tu," anafafanua Kitoboli.

Kitoboli anasema, kuna wanafunzi 270 waliokuwa wanabanana darasa moja, sasa wako huru, baada ya kukamilika vyumba vya madarasa katika maeneo yao.Anataja pingamizi walio nayo ni ubovu wa miundombinu kwa baadhi ya maeneo, hali inayosababisha kusuasua mipango na mikakati ya elimu kutokamilika kwa wakati.

Ofisa Elimu huyo, anataja kukosekana usafiri wa uhakika katika Idara ya Elimu, inakwamisha ufuatiliaji shughuli za maendeleo na utekelezaji malengo maalumu waliojiwekea katika kuzifikia shule.

### MSONGAMANO DARASANI

Kuhusu mafanikio, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Darajani, iliyopo kijiji cha Mkiwa, mpakani mwa Ikungi na Manyoni, Loth Ntandu, anasema shule yake imepunguza msongamano darasani na utoro, baada ya kugawanywa kutoka shule mama ya Mkiwa.

Anasema, wanafunzi hao wanafikia zaidi ya 360, wakwenda shule na kurudi nyumbani umbali wa kilomita 10, lakini baada ya jamii kuanzisha shule shikizi na Equip-T kujenga vyumba vya madarasa, itasajiliwa rasmi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kiupuiko, Mariam Makerah, anasema mpango wa Equip-T, umewainua, kutokana na kuimarika chombo 'Umoja wa Wazazi na Walimu' (UWW).

Anasema UWW ilianzishwa kupitia mradi wa EQUIP-T mwaka 2018, na umekuwa msaada katika kuimarisha taaluma shuleni hapo.

Mwalimu Mariam, anatoa mfano, kipindi serikali ilipofunga vyuo na shule nchini kutokana na tishio la ugonjwa wa corona, wazazi walilazimika kufanya kazi za shamba kupalilia alizeti na viazi vitamu kwenye shule yao, badala ya watoto.

Anasema, ni hali iliyotokana na umoja huo kubaini hatari mazao yao kuharibika katika kipindi watoto hawakuwepo, jambo walilolifurahia chini ya kivuli cha kinachoitwa "Mpango wa Kuinua Ubora wa Elimu Tanzania."

Emmanuel Msuta, anasema wanafanya kazi hiyo kwenye shamba la alizeti na viazi vitamu, huku wakiwa na tahadhari kubwa kutokana na ugonjwa wa corona, ikiwemo kuachiana nafasi ya kutosha kukwepa maambukizi.

Kwa mujibu wa mratibu wa Equip Tanzania, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Imani Maketa, mradi ulianza mwaka 2018 katika wilaya hiyo yenye shule za msingi 108 na sasa imefanikiwa kuimarisha sekta ya elimu ya msingi.

Ikungi ni wilaya iliyoanzishwa mwaka 2013 kutoka wilaya ya Singida, imefaulisha darasa la saba na kupanda kutoka nafasi ya tano mwaka 2017 na asilimia 66.38 kati ya halmashauri saba za mkoa wa Singida, hadi kushika nafasi ya nne mwaka jana (2019) sawa na asilimia 78.34.




Wanafunzi wa shule ya sekondari, wilayani Ikungi. **PICHA: MTANDAO.**

MAKALA

# Kenya inaposhtukia sasa corona Tanzania iling'amua mapema




Baadhi ya malori yakiwa yamesongamana mpakani wakati wa mapambano ya corona.

**Na Mwandishi Wetu**

NCHI ya Kenya imekuwa katika taharuki kubwa tangu kutangazwa kwa kisa cha kwanza cha Covid-19 mwezi Machi, mwaka huu.

Serikali ya nchi hiyo, imechukua hatua kali katika kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona, ikiwamo kuweka sheria ya kutotoka nje kwa baadhi ya maeneo, kuendesha upimaji wa nyumba kwa nyumba na kufunga mipaka yake kwa baadhi ya nchi jirani.

Katika kutekeleza hatua hizo, mara kadhaa kumeibuka migogoro ya mipaka kati ya Tanzania na Kenya, baada ya kuwazuia madereva kutoka Tanzania kwa kuhofia kusambaza ugonjwa huo.

Mgogoro huo uliposhika kasi, viongozi wakuu wa pande mbili, yaani Rais Dk. John Magufuli wa Tanzania na mwenzake wa Kenya, Uhuru Kenyatta, waliingilia kati kwa kutaka kuwapo na utulivu, huku utaratibu rafiki ukiandaliwa kwa ajili ya kuvusha bidhaa kutoka kila upande.

Hata hivyo, bado kulikuwapo na malalamiko ya uonevu kwa madereva kutoka Tanzania, ambao walilazimishwa kupimwa corona licha ya kuwa na vyeti vinavyoonyesha tayari wamepimwa na kuonekana hawana virusi vya corona.

Pamoja na mvutano huo, Tanzania, iliendelea kushikilia msimamo wake, kwamba haitafunga mipaka yake wala kuweka sheria za kuwazuia ndani watu kama njia ya kupambana na Covid 19, kwa sababu ugonjwa huo upo kwenye jamii na utaendelea kuwapo kwa muda mrefu.

Katika hotuba zake tofauti, Rais Magufuli, alisisitiza hawezi kuzuia shughuli za uchumi, akisema njia hiyo sio suluhu ya kupambana na virusi vya corona.

Mara kadhaa, Rais Magufuli, aliwatoa hofu wananchi na kuwahimiza wachape kazi mara dufu kwani virusi hivyo ni sehemu ya maisha ya kila siku, hivyo kumuamini Mungu na kufuata kanuni za afya ndio suluhu.

> **Mara kadhaa, Rais Magufuli, aliwatoa hofu wananchi na kuwahimiza wachape kazi mara dufu kwani virusi hivyo ni sehemu ya maisha ya kila siku, hivyo kumuamini Mungu na kufuata kanuni za afya ndio suluhu.**

### WAKENYA WENGI WANA CORONA

Pamoja na kuchukua hatua kali, ripoti mpya inaonyesha Wakenya milioni 2.6 tayari wana virusi vya corona, baada ya kupima damu zao.

Kulingana na ripoti hiyo, wanasayansi wamegundua hilo baada ya kupima damu iliyotolewa kwa ajili ya protini inayotumika kwenye mfumo kinga.

Protini hiyo (antibody) hutengenezwa na mwili kwa ajili ya kushambulia virusi na bakteria, na uwepo wake kwenye damu unaashiria kuwa mtu huyo hakuwahi kuwa na maambukizi.

Watafiti kutoka Taasisi ya utafiti wa tiba ya nchi hiyo, (kemri) wamechunguza sampuli za damu kutoka kwa watu waliochangia damu katika kampeni iliyofanyika nchi nzima kati ya miezi ya Aprili na Mei.

"Kupimwa kwa antibodies kumeonyesha kuwa Wakenya wengi tayari wamepata maambukizi, kuliko ilivyokuwa ikigundulika katika upimaji nchini humo," ulieleza utafiti huo.

Unaeleza baadhi ya watu inawezekana waliathirika mapema mwezi Machi, kutokana na protini hizo zinazopambana na virusi zinaweza kuwa kwenye damu kwa miezi kadhaa.

Kemri inakadiria kuwa karibu watu 550,000 jijini Nairobi na karibu 100,000 mjini Mombasa, tayari wameugua virusi hivyo na kupona na pengine kupata kinga.

Idadi hiyo inaonesha kuwa Wakenya wameshuhudia idadi kubwa ya watu waliopata maambukizi pamoja na vifo.

Taasisi hiyo ya utafiti ikikisia kuwa takriban watu 6,000 watakuwa wamepoteza maisha kutokana na ugonjwa wa Covid-19 katika nchi hiyo.

Kwa mujibu wa gazeti la The Standard media, sehemu ya ripoti ya taasisi ya Kemri ilisomeka kuwa katika mji kama Nairobi, idadi ya watu waliothibitishwa kuambukizwa wakati utafiti ulipokuwa ukifanyika ni 2,732 ikilinganishwa na idadi ya 550,000 wanaokisiwa kuwa na maambukizi. Mombasa katika takwimu ya sasa inaonyesha ni watu 1,368 waliopata Covid-19, lakini watu 100,000 wanakisiwa kuwa na maambukizi kutokana na utafiti huo.

"Namna nzuri ya kupima ili kujua walioambukizwa miongoni mwa raia wa Kenya ni kutembelea maeneo ya makazi kwa ajili ya kukusanya na kupima sampuli za damu". Inaongeza kusema taarifa hiyo.

Hata hivyo, upimaji wa aina hiyo haujaleta matokeo mazuri kwasababu ya masharti yaliyopo kutokana na hali ilivyo hivi sasa.

Mkurugenzi wa masomo ya sayansi na teknolojia kutoka Chuo kikuu cha Nairobi, Dk. Ayah, anasema kuwa idadi ya sampuli hizo ni ndogo kutathimini mwenendo wa maambukizi ya Covid-19.

### RAIS MAGUFULI ALIKUWA SAHIHI

Kulingana na matokeo ya utafiti huo, msimamo wa Rais Magufuli, wa kukataa kuweka mazuio kwa baadhi ya miji na kuzuia shughuli za kiuchumi ulikuwa sahihi.

Kiongozi huyo aliona hatua ya kuwazuia watu kufanya kazi na badala yake kuelekeza nguvu katika kupambana na virusi vya corona ni sawa na kuweka nchi katika hatari ya kuangamia na majanga mengine kama njaa na magonjwa.

HABARI KIMATAIFA

# Kim Jong-un asifu nchi yake kudhibiti corona

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

RAIS wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un, ameisifu nchi yake kwa kile alichokisema imepata mafanikio katika kukabiliana na Covid-19.

Kwa mujibu wa shirika la habari la taifa hilo KCNA, Kim alitoa kauli hiyo katika mkutano wa kamati kuu ya watunga sera wa Chama tawala cha kikomunisti unaofahamika kama Politburo, mjini Pyongyang.

Kiongozi hiyo alisema kuwa nchi hiyo ilizuia kusambaa kwa virusi hatari na kuimarisha hali ya usalama kwa watu wake.

Korea Kaskazini ilifunga mipaka yake na kuwaweka maelfu ya watu katika karantini miezi iliyopita wakati virusi viliposambaa duniani.

**Mafanikio katika kushughulikia virusi yalifikiwa kutokana na uongozi unaoona mbali wa Kamati Kuu ya Chama hicho.**

Nchi hiyo, ilidai kuwa haikuwa na virusi vya corona, ingawa wachambuzi wanasema huenda isiwe sahihi.

Kim (pichani) anasemekana alitathmini kwa kina miezi sita ya kukabiliana na janga

Alisema mafanikio katika kushughulikia virusi yalifikiwa kutokana na uongozi unaoona mbali wa Kamati Kuu ya Chama hicho.

Lakini alisisitiza umuhimu wa kuimarisha tahadhari ya hali ya juu bila kulegeza katika mapambano dhidi ya janga hilo.

Aidha alitoa onyo kwamba kulegezwa kwa hatua za kupambana na corona kutasababisha mzozo usiofikirika na ambao hauwezi kutatuliwa .



Shirikisho la kimataifa la msalaba mwekundu, lina wahudumu wa kujitolea katika eneo la mpakani wanaotoa huduma ya hatua za kuzuia maambukizi ya virusi na kumekuwa na ripoti kadhaa ambazo hazijathibitishwa za watu wenye virusi ndani ya nchi hiyo.

Lakini taarifa nyingi kuhusu maisha katika mji mkuu wa nchi hiyo, zilizotolewa katika wiki za hivi karibuni zinaonyesha kuwa maisha yanaendelea kama kawaida

Mwishoni mwa mwezi Januari, Korea Kaskazini ilichukua hatua za haraka dhidi ya virusi kwa kufunga mipaka yake na baadaye kuwaweka katika karantini mamia ya wageni katika mji mkuu, Pyongyang. **BBC**



Waokoaji wakitoa miili ya wachimbaji waliokufa ndani ya mgodi wa madini ya Jade katika mji wa Hpakhant, jumla ya maiti 120 ziliopolewa baada ya kutokea maporomoko kwenye mgodi huo uliopo Kaskasini mwa Myanmar. **PICHA: AFP**

## Kinara wa maandamano akimbia Hong Kong

**HONG KONG,** China

KINARA wa waandamanaji na mwanaharakati wa kupigania demokrasia wa Hong Kong, Nathan Law, ameukimbia mji huo na kwenda katika eneo lisilojulikana.

Hatua ya kwenda mafichoni imekuja baada ya kutoa ushahidi mbele ya wabunge wa Marekani dhidi ya sheria kali ya usalama iliyotangazwa na China hivi karibuni.

Sheria hiyo ambayo imeibua maandamano katika mji huo, inapunguza kwa kiasi kikubwa haki ya kiraia.

Katika ujumbe wake kupitia mtandao wa Facebook aliochapisha juzi usiku, Law alisema ameamua kuitetea Hong Kong kimataifa na ameuhama mji huo.

Law aliondoka Hong Kong siku mbili baada ya sheria hiyo ya usalama wa kitaifa kuanza kutekelezwa. **DW**

## Mtandao wadukuliwa, 746 wakamatwa

**LONDON,** Uingereza

HATIMAYE mfumo wa mawasiliano wa siri unaotumiwa na wahalifu wa biashara haramu ya mihadarati na silaha umenaswa.

Mfumo huo uligunduliwa na Shirika la kupambana na uhalifu la Uingereza lililoshirikiana na vikosi vya maeneo ya Ulaya, baada ya kufanyika kwa oparesheni maalum nchini humo.

Watu 746 walikamatwa katika nchi mbalimbali za Ulaya baada ya ujumbe kwenye mtandao wa mawasiliano wa EncroChat kudukuliwa na kurekodiwa.

Kati ya vitu vilivyokamatwa baada ya kufuatiliwa kwa ujumbe huo ni tani mbili za dawa za kulevya, bunduki kadhaa na pauni milioni 54.

Maofisa walisema walifanikiwa kuzuia watu kadhaa kuuawa baada ya kufuatilia mashambulio yaliyokuwa yamepangwa na ujumbe wa kutishia maisha katika mfumo huo wa mawasiliano.

Shirika hilo limesema kuwa oparesheni hiyo ilifanyika kwa muda wa zaidi ya miezi mitatu, ikijumuisha polisi wa Uingereza.

Kubainika kwa mtandao huo kumeleta athari kwa magenge yanayopanga uhalifu ambayo hayajawahi kushuhudiwa.

Kamishna wa polisi, Dame Cressida Dick, alisema kikosi chake pekee kilikamata watu 132 na kunasa pesa taslimu pauni milioni 13.3. Inasemekana kwamba watu 60,000 miongoni mwao raia 10,000 wa Uingereza, walijiandikisha kupokea huduma za mtandao wa EncroChat ambao makao yake ni Ufaransa, lakini kwa sasa imefutwa kabisa.

Mfumo huo wa mawasiliano ulifanyakazi katika simu janja na kulingana na tovuti ya mtandao huo, ilitoa huduma ya usalama wa mawasiliano bila malipo.

Wateja walikuwa wanaweza kupata huduma kama ujumbe mbaya uliofutika kutoka kwa simu ya aliyeupokea baada ya kipindi fulani.

Pia ulikuwa unaweza kufuta data zote kwenye kifaa kama simu kwa kuingiza msimbo yaani neno la siri kwa lugha ya kiingereza ya namba nne kutoka kwa skrini iliyojifunga. **BBC**

## Castex ateuliwa Waziri Mkuu

**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amemteua Jean Castex, kuwa Waziri Mkuu mpya.

Taarifa kutoka Ikulu ya Ufaransa inayofahamika kama , Elysee, imesema Castex (55), kabla ya uteuzi huo alikuwa kiongozi wa mkakati wa kupunguza hatua za kuzuia kuenea virusi vya corona. Macron amemuagiza Castex (pichani), kuunda serikali haraka. Uteuzi wa Castex umeufanya baada ya aliyekuwa Waziri Mkuu, Edouard Philippe, pamoja na serikali yake yote kutangaza kujiuzulu jana.



Hatua hiyo, inafuatia ahadi ya Macron kulifanyia mageuzi baraza lake la mawaziri baada ya chama chake kufanya vibaya katika uchaguzi wa manispaa wiki iliyopita. Kujiuzulu kwa Philippe, kunampa nafasi Rais Macron kuijenga upya timu atakayoingia nayo katika uchaguzi utakaofanyika mwaka 2022.

Hata hivyo, serikali ya sasa itaendesha shughuli za dharura hadi baraza jipya la mawaziri litakapoapishwa. **DW**


# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini- 19

Mtunzi anapatikana (0716 350534)




Na Adam Fungamwango

ILISEMWA hapo zamani kuwa, dunia inaharibiwa na vitu viwili tu, mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

"Hivi kwa nini?" Lilikuwa ni swali kutoka kwa Shani lililoulizwa kwa sauti ndogo na ya chini, tofauti na maongezi ya mwanzo, ambalo lilionekana kumshagaza kidogo Eddy.

"Kwa nini vipi?" Eddy naye badala ya kujibu aliuliza kwa mshangao.

"Hata mimi sielewi kwa kweli." Shali aliongeza mshangao kwenye akili ya Eddy.

"Hebu wewe niambie kwa nini?" Eddy alihamisha swali aliloulizwa na muulizaji, kutoka kwa muulizwaji kwenda tena kwa muulizaji."

"Ikipita siku hatujawasiliana inakuwa kama mwezi hivi. Hizi siku nne ambazo hatujawasiliana kwangu ilikuwa ni kama miaka minne." Shani alionekana kujibu swali ambalo alimuuliza Eddy, lakini kwa utaalam, hasa kutokana na kazi yake, alilirudisha kwake na kujikuta akijibu.

"Mimi tusipowasiliana siku moja nakuwa kama naumwa." Alijibu Eddy

"Muongo, mbona siku nne hakujanipigia wala kunitumia meseji?"

"Nilikwambia, nilikuwa kibaruani, huwa sipendi kuongea na wewe kijuujuu. Napenda niwe nimetulia. Tuongee maneno ya furaha, tukiwa tumetulia." Jibu hilo lilionekana kumtuliza Shani.

"Mmh, lakini wewe utakuwa ni sababu." Shani alisema na maneno hayo yalipenya hadi kwenye moyo wa Eddy, akasikia kusisimkwa na mapigo ya moyo kuongezeka.

"Hata mimi ninavyojisikia, sababu itakuwa ni wewe." Eddy naye alirudisha mapigo.

"Unajisikiaje?" Shani aliendelea kuwa mchokozi.

"Nasikia kama kuna kitu rohoni hivi."

"Kitu gani hicho?"

"Sijakijua, ila ngoja nikitafute, nikikipata nitakwambia, lakini ukweli ni kwamba nikikuona au kuwasiliana na wewe nasikia raha sana, ila nisipowasiliana na wewe au kukuona nakuwa kama yatima vile." Eddy naye ni kama alichokozwa hivi. Akawa anatema nyongo.

"Hahahaha haya bwana, kitafute hicho kitu, halafu uniambie." Shani alisema akionekana kufurahia maneno ya Eddy. Naye alihisi kitu kama msisimko mwilini, huku joto likiongezeka mwilini.

"Hiki kitu naona tukitafute wote. Nisaidie kukisaka. Tukikipata chetu wote." Alisema Eddy na alipomaliza alisikia kicheko kutoka upande wa pili wa simu. Maneno yalimfurahisha mno Shani. Eddy naye akajikuta anacheka. Wakaangua kicheko pamoja.

"Hahahaha, haya bwana kitafute hicho kitu, halafu uniambie." Shani aliendelea kumchokoza Eddy.

"Hiki kitu naona tutafute wote. Nisaidie kukisaka, halafu tukikipata chetu wote." Eddy alizidi kuchokozeka.

"Ila kwa upande wangu wewe ndiyo sababu. Mimi muda wote nawaza kutaka kuongea na wewe. Huwa nafurahi sana nikikuta meseji yangu, hasa pale siku za mwanzo ulipotoka huku, lakini baadaye nikaona umenisahau."

Eddy alicheka kidogo na kuongea. "Wewe hunishindi mimi kukuwaza."

"We mimi nakushinda, siku hizi hunitumii meseji, sijui unasema una kibarua kimekuweka bize, siku ile ulipotoka kwangu, ilikuwa kila siku asubuhi unanitumia meseji, basi nilikuwa nafurahi sana, siku nisipoona nawaza kuna nini? Lakini siku hizi..."

Hapo Eddy alijua kuwa yalikuwa ni malalamiko. Malalamiko yaliyotokana na mazoea. Anakumbuka siku ile alipoalikwa na Shani, ilikuwa asubuhi ni lazima amtumie meseji ya kumsalimia na kumtania kama kawaida yake, kabla ya kufanya chochote.

Tayari alijua ana kazi ya kufanya.

"Kwa nini ukiona meseji yangu unafurahi sana?" Lilikuwa ni swali ya uchokonozi kutoka kwa Eddy.

"Mimi nahisi upendo, wewe unahisi nini?" Lilikuwa ni jibu lililochanganyikana na swali. Tena la mtego.

"Upendo si ndiyo mapenzi? Au mimi nachanganya madawa?" Hilo lilikuwa ni swali jibu, halafu lililotengenezwa kiufundi kabisa na Eddy.

"Mmmh, hapo mimi sasa sielewi, ndiyo maana nimekuuliza wewe." Shani alikwepa swali la kiufundi.

Eddy alijua hilo, akaangua kicheko na na kusema.

"Hahahaha, upendo ndiyo hayo hayo mapenzi, ila mimi naona upendo umezidi kwako. Yaani nakupenda sana."

Kulitokea ukimya wa ghafla baada ya maneno hayo kwa wote wawili. Baada ya nusu dakika Shani aliuvunja na kuguna

"Duh."

"Mbona umeshtuka?" Eddy aliuliza.

"Hapana. Nimefurahi tu." Shani alijibu.

"Unanicheka eee, poa tu Mungu yupo."

"Sijakucheka bwana. Nimefurahi tu, kwa sababu hata mimi najisikia kama wewe." Shani alijibu na kushusha pumzi ambayo hata Eddy aliisikia kwenye simu yake.

"Pole sana." Eddy aliongeza.

"Kwa nini sasa hukuniambia sasa tokea mwanzo ulivyoanza kujihisi hivi kwangu mimi?" Shani alionekana bado kutaka kujua kitu.

"Shani, kila kitu kina muda wake, ilibidi kwanza nijidhihirishe kama nakupenda au nakutamani tu. Ila sasa nimeamini kuwa nakupenda kutoka rohoni."

"Okay, nimekuelewa Eddy."

"Poa, basi nikutakie mchana mwema."

"Okay kazi njema Eddy."

"Na kwako pia."

"Nakupenda." Kwa mara ya kwanza Shani alitamka neno hilo kwa Eddy.

Kwa upande wake Eddy alitabasamu na kuona sasa kazi ya kumtia mkononi mrembo Shani ilikuwa imekamilika. Kwa muda mfupi tu walipoonana, aliondokea kumhusudu sana.

"Nami pia nakupenda sana." Eddy alijibu.

"Nakuomba Jumamosi uje kwenye hoteli ya ABC Club Mbezi Beach ili tufurahi kwa pamoja, tujipongeze."

"Omba kingine mpenzi, hilo limepita bila kupingwa." Eddy alijibu, maongezi yakaisha na kukata simu zao.

**Ila kwa upande wangu wewe ndiyo sababu. Mimi muda wote nawaza kutaka kuongea na wewe. Huwa nafurahi sana nikikuta meseji yangu, hasa pale siku za mwanzo ulipotoka huku, lakini baadaye nikaona umenisahau.**

ITAENDELEA JUMAMOSI

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO-MJINI**
**WILAYA YA DODOMA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**SHAURI LA MADAI 188, 190, 192, 193, 195, 196, 198 na 199 YA 2020.**
**MDAI………….DODOMA PESA LTD**
**DHIDI YA**

**WADAIWA………..1. MUSTAFA ALLY MISANYA/KORETA JACOB, 2. HUSNA HUSSEIN ISSA, 3. ALESI LEONARD MADINDA, 4. RICHARD LEONARD BUZUYA, 5. MAGRETH NDALU NDAHANI, 6. CHIKALISA RAMADHANI, 7. ZAIUNI ATHUMANI MAHUMBI, 8. HAPPINESS PIUS MWIHAMBI.**

Kwa kuwa mdai mtajwa hapo juu alifungua mashauri didhi yenu wadaiwa watajwa hapo juu. Mnaarifiwa na Jamhuri kuhudhuria mbele ya Mahakama hii mnamo tarehe 06/07/2020 bila kukosa ili kuja kujibu madai hayo dhidi yenu. Endapo hamtahudhuria mbele ya mahakama siku hiyo shauri/mashauri hayo yatasikilizwa upande mmoja (Exparte Hearing) na kutolewa maamuzi. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Mahakama hii leo tarehe 02/07/2020.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO-MJINI
DODOMA

158004

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLEN MWAKYOMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 390 BAG aina ya LEYLAND ALBION rangi ya murtcolour, Engine namba 97202D. Chassis namba E0402320287945733.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: MB/RB/116246/2018.

15800302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SOCIETY OF THE PRECIOUS BLOOD inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 646 ACZ TOYOTA LAND CRUSSER. Chassis namba JT711PJA507004987. Engine namba IHZ 0277035.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi: WMB/RB/708/2020.

15799602

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5
KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;171/2020**

Ombi la MIRAJI ISSA MUHANGE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HUSSEIN ALLY MAJEMANGA Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 14/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/07/2020.

Sahihi ya Hakimu

15800002

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5

KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;151/2020**

Ombi la **HAMADI JEREMIA NYAMNYAM** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu BAHATI JOHN KAMBALENJA Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/06/2020.

Sahihi ya Hakimu

15799902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KARAGWE KAYANGA**
**MAOMBI NA. 04/2020**
**MARCIANA GEORGE……………….MWOMBAJI**

**DHIDI YA**
**KARAGWE DISTRICT COUNCIL**
**LUCY STEPHEN**
**EGIDIUS BASHAIJA……………..WAJIBU MAOMBI**

**KWA: EGIDIUS BASHAIJA – (POPOTE PALE ALIPO)**

Unaarifiwa kuwa Maombi Na. 04/2020 yamepangwa kutajwa tarehe 24/7/2020 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, J.K. BANTURAKI saa 2:00 asubuhi, mahali – KAYANGA – KARAGWE. Hivyo unaamriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 22/5/2020.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**KAYANGA - KARAGWE**

15800102


**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# KLOPP ATABIRI LIVERPOOL ITAVUNJA REKODI YA MAN CITY

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema Liverpool bado ina malengo ya kuipiku rekodi ya Manchester City ya kufikisha poiti 100 kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

City iliweka rekodi ya kufikisha pointi 100 wakati wa msimu wa 2017/18, tayari Liverpool wameshatwaa taji la ligi hiyo msimu huu.

Hata hivyo, kikosi hicho cha Klopp kilikutana na kipigo kizito cha mabao 4-0 kutoka kwa City ya Pep Guardiola, Alhamisi, kikiwa ni kichapo chao cha pili msimu huu kwenye ligi.

Liverpool inaweza kufikisha pointi 104 msimu huu kama kikosi hicho cha Klopp kitashinda mechi zake zote sita zilizobaki.

"Angalia, ilivyotokea, lakini hatuwezi kulazimisha hilo. Kwenda pale kushinda mechi zote, tunatakiwa kushinda mechi zilizobaki na hatukufanya hivyo dhidi ya City," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Hivyo, katika kitu cha kwanza, sasa tunatakiwa kujua kwamba tupo tayari kwa mchezo unaofuata dhidi ya Aston Villa. Jumla ya pointi tutakazopata msimu huu ni matokeo ya kile tulichokipata katika kila mchezo."

Liverpool imebakiza mechi dhidi ya Villa, Brighton and Hove Albion, Burnley, Arsenal, Chelsea na Newcastle United kabla ya msimu kumalizika.



# Guardiola afunguka kuhusu msimu ujao utakavyokuwa

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola ameonya kuwa msimu ujao wa Ligi Kuu England "unaweza kuwa tofauti kabisa" huku Manchester City ikijipanga kulitwaa taji hilo.

City walikuwa na kiwango kizuri wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya mabingwa Liverpool kwenye mchezo uliopigwa pale Uwanja wa Etihad, Alhamisi.

Penalti ya Kevin De Bruyne na mabao kutoka kwa Raheem Sterling na Phil Foden na lile la kujifunga la Alex Oxlade-Chamberlain, ilishuhudia City - mabingwa wa msimu wa 2017/18 na 2018/19 wakipata ushindi huo mtamu.

Huku Guardiola akizungumzia athari ya msimu ujao, kocha huyo wa City alisema msimu wa 2020/21 unaweza kuwa tofauti.

"Nina furaha tumeshinda dhidi ya timu ambayo ni bingwa wa Ulaya na England," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Walikuwa na nafasi ya kutufunga. Niliona sura zao, namna walivyopiga kelele, namna walivyokuwa wanawasiliana, jinsi walivyokuwa wanaonyesha nia yao ya kutufunga.

"Hawakuja tu hapa kusherekea, watakwenda kusheherekea. Nafikiri walikunywa bia nyingi mapema wiki hii, lakini walikuja hapa kushinda dhidi yetu sisi, bila shaka yoyote.

# Zidane amtaka Messi kubaki Barcelona

**MADRID,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane anataka nyota wa Barcelona, Lionel Messi kubaki kwenye LaLiga wakati huu kukiwa na uvumi juu ya uwezekano wa yeye kuondoka.

Messi mwenye umri wa miaka 33, mkataba wake na Barca unamalizika mwaka 2021 lakini kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari vya Hispania juzi Alhamisi, vimedai mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or anafikiria kuondoka.

Kwa mujibu wa Cadena SER, Messi amesitisha mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya kutokana na kutoelewa kinachoendelea hapo Barca ambao wanaonekana kuzidiwa na wapinzani wao Madrid kwenye mbio za ubingwa msimu huu.

Zidane aliulizwa kuhusu uvumi unaomhusu Messi baada ya Madrid kupaa kileleni kwa pointi nne dhidi ya Barca shukrani kwa ushindi wa Alhamisi wa bao 1-0 dhidi ya Getafe.

"Sijui nini kitatokea, lakini tuna matumaini kwamba atabakia kwenye ligi kwa sababu yeye mwenyewe anataka kucheza katika ligi bora duniani," alisema Zidane baada ya mchezo huo.

Sergio Ramos alikuwa shujaa wa Madrid dhidi ya Getafe, akifunga bao hilo pekee kwenye mchezo huo kwa mkwaju wa penalti dakika ya 79, mchezo uliopigwa dimba la Alfredo di Stefano.

Huo ulikuwa ni ushindi wa sita mfululizo kwa Madrid wakati Los Blancos wakiongeza nafasi ya kuliwania taji la LaLiga dhidi ya Barca, huku zikiwa zimesalia mechi tano msimu kumalizika.

Zidane pia alimsifia nahodha wake, Ramos, ambaye sasa alifikisha mabao tisa aliyofunga kwenye LaLiga kwa msimu huu 2019-20 akiwa anacheza mechi yake ya 450 kwenye ligi hapo Madrid.



HABARI MICHEZO

# Carvajal awakabidhi taji la LaLiga Madrid

**MADRID,** Hipania

MLINZI wa Real Madrid, Dani Carvajal, amesema Los Blancos hao wapo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kushinda taji la LaLiga msimu huu baada ya ushindi walioupata wa bao 1-0 dhidi ya Getafe.

Madrid walipaa kileleni kwa pointi nne zaidi dhidi ya wapinzani wao Barcelona shukrani kwa ushindi wa Alhamisi, mchezo uliopigwa pale kwenye dimba dogo la Alfredo di Stefano.

Sergio Ramos alifunga penalti dakika ya 79 na kuwafanya Madrid kupata ushindi wa sita mfululizo tangu kurudi kwa msimu huu baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Madrid haijashinda taji la LaLiga tangu msimu wa 2016/17, lakini sasa kikosi hicho cha kocha, Zinedine Zidane kipo kwenye nafasi nzuri ya kumaliza utawala wa Barca huku zikiwa zimesalia mechi tano ligi kumalizika.

"Ni wazi kwamba tuna faida ya pointi nne zaidi kileleni na sasa itategemea sisi wenyewe kushinda ligi. Tupo kwenye nafasi nzuri," alisema Carvajal, ambaye ndiye aliyezawadiwa penalti hiyo baada ya kuangushwa na mlinzi wa Getafe, Mathias Olivera.

"Getafe ilicheza vizuri kwa kipindi chote cha mchezo. Tulitumia nafasi ya kuteleza kwa Barcelona, ulikuwa kama mchezo wa fainali.

"Getafe waliufanya mchezo kuwa mgumu sana kwetu. Tulitakiwa kuwa makini na kujituma na kuonyesha umoja wetu."







# HAKIMI ASAJILIWA RASMI INTER

**MILAN,** Italia

ACHRAF Hakimi amejiunga na Inter Milan kwa mkataba wa kudumu akitokea Real Madrid, klabu hiyo ya Italia imethibitisha.

Hakimi mwenye umri wa miaka 21, ameripotiwa kukigharimu kikosi hicho cha kocha, Antonio Conte kiasi cha euro milioni 40 na amejiunga nao kwa mkataba wa miaka mitano. Taarifa ya Madrid ilisomeka: "Klabu inataka kumshukuru Achraf kwa miaka aliyokuwa hapa, kwa namna alivyojitoa na tabia yake nzuri aliyoionyesha tangu alipotua hapa kwenye akademi mwaka 2006 na tunamtakia kila la heri katika maisha yake mapya."

Mzaliwa huyo wa Hispania raia wa Morocco ametumia misimu miwili akicheza kwa mkopo kwa miamba wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Borussia Dortmund na alionyesha kiwango bora kabisa.

Pamoja na hilo, alifunga mabao matano, na kutoa pasi za mwisho 10 kwenye Bundesliga msimu huu akiwa mlinzi bora zaidi, alikuwa na mchango mkubwa kwa timu.

Dortmund walitaka kumbakiza Hakimi pale kwenye dimba la Signal Iduna Park, lakini waliamua kumwachia baada ya kufanikiwa kumsajili Thomas Meunier kwa uhamisho huru akitokea Paris Saint-Germain.

Hakimi amekuwa pale Madrid tangu mwaka 2006 na aliingia kwenye kikosi cha kwanza msimu wa 2017-18, akicheza kama msaidizi wa Dani Carvajal.

# *Arteta matumaini kwa Aubameyang*

**LONDON,** England

MIKEL Arteta anaamini Pierre-Emerick Aubameyang ni muhimu kwa Arsenal kama ilivyokuwa kwa Robin van Persie wakati akiwachezea miamba hao wa London Kaskazini.

Aubameyang alikuwa mchezaji wa haraka zaidi kwa Arsenal kufikisha mabao 50 kwenye Ligi Kuu Jumatano, akifikisha mechi 79 kwenye ligi hiyo wakati washikabunduki hao wakiwafumua Norwich City mabao 4-0.

Baada ya mchezo huo, Arteta alidai "alikuwa chanya sana" kwamba straika huyo mwenye miaka 31 anaweza kukubali kuongeza mkataba wake hapo kwenye dimba la Emirates, huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu ujao.

Akizungumza na waandishi wa habari kuelekea mchezo wa wikendi hii dhidi ya Wolves, Arteta alisema ana imani nyota huyo anaweza kukubali kubakia hapo.

"Sijui ni namna ninavyojisikia," alisema. "Namna ninavyowasiliana nae, majadiliano ninayofanya nae, na watu waliomzunguka. Ina nipa nguvu kuamini kwamba mambo yanaweza kuwa shwari.

"Huu ni mtazamo wangu mimi. Vitu vinabadilika haraka sana kwenye soka, lakini kama ukiniuliza mimi namna gani najihisi kuhusu majaliwa ya Auba kwa wakati huu, nahisi kwamba anataka kuendelea kuwa na sisi na kuendelea kuimarika na kutusaidia kuwa timu bora."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BAYERN RASMI YAMSAJILI SANE

Winga huyo Mjerumani afunguka amejiandaa kupambana na changamoto...

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich imethibitisha imemsajili Leroy Sane kwa dau la pauni milioni 55, saa chache baada ya vigogo hao wa Ujerumani kulazimishwa kuomba radhi kwa sababu ya kuweka hadharani picha za winga huyo akiwa amesaini mkataba na klabu hiyo, ikiwa ni kabla ya taarifa rasmi kutolewa.

**Sane amesaini mkataba wa miaka mitano wa kuwatumikia mabingwa hao wa Bundesliga, ambao utamalizika ifikapo Juni, 2025.**

Lakini kabla klabu hiyo haijathibitisha kukamilisha mchakato huo wa usajili, picha rasmi za winga huyo mwenye umri wa miaka 24 akionekana anasaini mkataba zilionekana kwenye mtandao wa Bayern wenye kuandikwa kwa lugha ya kiarabu hapo juzi, muda mfupi baadaye ndio wakaweka katika akaunti za mitandao ya kijamii za klabu hiyo.

Huku usajili huo wa Sane ukionekana umefanikiwa, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani anasisitiza anasubiri kwa hamu kukutana na changamoto mpya kwenye klabu hiyo ambayo ni ya ardhi aliyozaliwa.

Sane alisema katika mtandao wa Bayern: "FC Bayern ni klabu kubwa yenye malengo makubwa, na malengo hayo ndiyo yaliyonileta hapa. Niko tayari kupambana na changamoto mpya na ninasubiri kwa hamu kuanza mazoezi ya pamoja.

"Ninamjua Hansi Flick tangu nilipokuwa na Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 21 (U-21), tuna uhusiano mzuri sana tulipokuwa kwenye timu hiyo. Ninataka kushinda vikombe mbalimbali ikiwezekana nikiwa na FC Bayern, na taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya ndio lengo langu kubwa."

Sane pia aliwashukuru mashabiki wa City kwa ushirikiano waliompa kwa muda wote aliokuwa hapo, baada ya kuitumikia klabu hiyo kwa muda wa miaka minne.

" Nashukuru sana kwa kuwa na wakati mzuri na kwa ushirikiano mlionipa wa miaka minne. Ulikuwa ni wakati mzuri na wenye mafanikio ambayo sitaweza kuyasahau. Tulishinda mechi nyingi, tulifunga idadi kubwa ya mabao, tulivunja rekodi mbalimbali na tulisheherekea vikombe pamoja.

"Nawashukuru sana mashabiki wote, wafanyakazi na wachezaji wenzangu! Kila siku nitaendelea kukumbuka wakati huu mzuri tuliokuwa pamoja kwa furaha na kujivunia. Pia ninamshukuru kocha wangu kwa kunifanya kuwa mchezaji mzuri na kufikia kushinda tuzo ya Mchezaji Bora Chipukizi mwaka 2018. Nimejifunza vitu vingi na ninajivunia kuwa sehemu ya safari ya mafanikio." Sane aliandika katika ukurasa wake wa Twitter.

Majira ya joto mwaka jana, thamani ya Sane ilitajwa kuwa ni zaidi ya pauni milioni 130, wakati klabu mbili zikiwania saini yake, kabla ya kupata majeraha katika mchezo wa Ngao ya Jamii na kusababisha dili hilo kusitishwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bayern, Karl-Heinz Rummenigge aliongeza wanajisikia furaha kukamilisha mchakato huo wa Sane kutua Allianz Arena, baada ya kuhusishwa naye tangu majira ya joto mwaka jana.

Kiongozi huyo aliongeza: " Tunafuraha sana kumkaribisha Leroy Sané hapa Bayern. Ni mchezaji ambaye ana uwezo na amethibitisha kiwango chake kwa miaka ya hivi karibuni, hasa akiwa kwenye Timu ya Taifa.

## ZISIKUPITE

### BAILEY ANUKIA ENGLAND

EVERTON, Liverpool, Manchester City na Manchester United zote zinatarajia kumfuatilia winga wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Jamaica, Leon Bailey (22), katika mechi yake ya ligi itakayochezwa leo, huku winga huyo akionekana anajiandaa kuhamia England. ***(Sky Sports)***

### ALCANTARA KUTUA LIVERPOOL

MABINGWA wapya wa Ligi Kuu England, Liverpool, wanakaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili kiungo wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Hispania, Thiago Alcantara, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Sport)***

### KLOPP AMTAKA CAKIR

LIVERPOOL pia imetajwa kuwania saini ya golikipa wa Trabzonspor na Timu ya Taifa ya Uturuki, Ugurcan Cakir, ambaye ana umri wa miaka 24. Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp amevutiwa na mlinda mlango huyo. ***(Talksport)***

### KOULIBALY ATAJWA CITY

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amewataja nyota anaowahitaji ni beki wa Napoli Msenegal, Kalidou Koulibaly (29), nyota wa Villarreal na Timu ya Taifa ya Hispania, Pau Torres (23), na beki wa Benfica na Ureno, Ruben Dias (23), ili kuijenga upya safu yake ya ulinzi. ***(Times - subscription required)***

### ARRIZABALAGA ANUKIA SEVILLA

SEVILLA imemweka katika orodha ya wachezaji inaowahitaji golikipa wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Hispania, Kepa Arrizabalaga (25), ambaye bado hatima yake katika kikosi cha Stamford Bridge haijulikani. ***(Sun)***

### VALENCIA YAMTAKA BAILLY

MANCHESTER United imefungua milango kwa mchezaji wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Eric Bailly (26), kuondoka klabuni hapo msimu ujao, huku klabu ya La Liga, Valencia ikionekana kuhitaji huduma ya beki huyo. ***(Sun)***

### HENDERSON AIONYA UNITED

GOLIKIPA wa Manchester United, Dean Henderson, ambaye yuko kwa mkopo Sheffield United, ameionya klabu hiyo ya Old Trafford kuwa hataweza kusubiri kwa muda usiojulikana kuwa kipa chaguo la kwanza, huku kukiwa na tetesi za kutakiwa na Chelsea. ***(Express)***

### MAIGNAN ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA inajiandaa kumsajili golikipa wa Lille Mfaransa, Mike Maignan (24), pamoja na Alphonse Areola (27), ambaye yuko kwa mkopo Real Madrid akitokea Paris St-Germain. ***(Express)***

### MAIGNAN KUMRITHI LLORIS

TOTTENHAM inaongeza nguvu katika mchakato wa kuwania saini ya Mike Maignan, huku Kocha Jose Mourinho akimtaja nyota huyo anakwenda kuziba nafasi ya golikipa wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Hugo Lloris, 33. ***(Sun)***

### BARKLEY ATAJWA WEST

KOCHA wa West Ham, David Moyes, amefufua upya mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Ross Barkley (26). The Blues ilikataa ofa ya Hammer kuhusu mchezaji huyo iliyowasilishwa katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

## Wanariadha Dar kuchuana Uhuru

**Na Shufaa Lyimo**

WANARIADHA kutoka klabu mbalimbali wanatarajia kuchuana katika mashindano ya wazi yatakayofanyika leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana ,Kocha Mkuu wa timu ya riadha mkoa wa Dar es Salaam, Idd Muhunzi, alisema lengo la mashindano hayo ni kuangalia uwezo wa kila mchezaji baada ya kukaa muda mrefu kutokana na kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona.

"Mashindano hayo yatashirikisha klabu mbalimbali zikiwamo zile timu za Umiseta ambazo zilishiriki mashindano ya Taifa mwaka jana," alisema Muhunzi.

Kocha huyo alisema wachezaji watakaokuwa na uwezo mzuri watapata nafasi ya kushiriki katika mashindano ya Taifa yatakayofanyika kuanzia September 5 na 6, mwaka huu.

" Ugonjwa wa corona ulituvurugia mipango mingi, isipokuwa bado naamini wachezaji wangu watakuwa katika kiwango bora kama awali, licha ya kukaa muda mrefu bila kushiriki mashindano yoyote," Muhunzi alisema.

Aliwataka wadau wa mchezo huo kujitokeza kushuhudia wachezaji watakaokuwa wanashiriki mashindano hayo ili kuongeza hamasa katika mchezo huo.

## KMKM yaifanyia 'mauaji' Malindi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KIKOSI cha Mabaharia wa KMKMK kimeichapa bila huruma Mlandege mabao 5-0 katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Mau A visiwani hapa.

Kwa Matokeo hayo, Malindi imeendelea kusalia katika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar wakiwa na alama 31, KMKM wakitinga kileleni mwa msimamo huo kwa kishindo wakiwa na alama 49.

Kocha Msaidizi wa Malindi, Waziri Seif, ameliambia gazeti hili matokeo mabaya ya timu yake katika mchezo huo yametokana na wachezaji wake kutofanya mazoezi kikamilifu ya kuendelea na ligi hiyo iliyosimama zaidi ya miezi mitatu.

Seif alisema kikosi chake kilishindwa kuhimili ushindani wa mechi hiyo ambayo waliipoteza kwa kufungwa idadi kubwa ya mabao.

Hata hivyo aliahidi watarejea kwenye ushindani kwa kufanya mazoezi kwa bidii ili kusaka pointi kwenye mechi zinazofuata.

"Ipo haja kwa wachezaji kufanya mazoezi ili timu icheze vizuri kama ilivyokuwa hapo awali, wachezaji walicheza vizuri sana ila walizidiwa kutokana na kutofanya mazoezi inavyotakiwa,"alisema.

Bado nafasi ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu wa 2019/20 iko wazi huku KMKM na Mlandege zikikimbizana.

# SIMBA QUEENS YAPANIA KUVUNJA REKODI YA JKT

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutoa kichapo cha mabao 10-0 kwa Panama Girls, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' amesema malengo yao ni kupambana ili kuhakikisha wanatwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu wa 2019/20, bila ya kufungwa na timu yoyote.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mgosi, alisema wamejipanga kufanya vizuri katika mechi zote zilizosalia za ligi hiyo inayochezwa kwa mfumo wa nyumbani na ugenini.**

Mgosi alisema endapo watashinda mechi zote, hesabu zake za kutwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu zitakuwa zimetimia.

"Msimu huu tumedhamiria kutwaa ubingwa, tunajipanga vizuri kuhakikisha tunapata pointi muhimu kwa kushinda mechi zetu zote zilizobaki ikiwamo mechi yetu ijayo dhidi ya JKT Queens," alisema Mgosi.

Kocha huyo alisema ana waheshimu wapinzani wao, ana imani mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kutokana na kila timu kuhitaji kutimiza malengo yake.

"JKT Queens ni timu nzuri, ninawaheshimu wapinzani wetu, ila tunarejea nyumbani kufanyia kazi upungufu wetu ili kufikia malengo yetu ya kutwaa kikombe cha ligi bila kufungwa katika mechi zilizobakia," alisema Mgosi.

Aliongeza kikosi chake kipo vizuri na kila siku wachezaji wake wanaahidi kuendelea kupambana ili kutimiza ndoto za kutwaa ubingwa kwa mara ya kwanza.

"Baada ya kupata matokeo mazuri katika mchezo wetu dhidi ya Panama, sasa tunarejea kujiandaa na michezo yetu miwili (JKT Queens na Yanga Princess), tutakayocheza nyumbani Simba Mo Arena," Mgosi alisema.

Simba Queens iliendelea kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania kwa kufikisha pointi 35 wakifuatiwa na mabingwa watetezi, JKT Queens wenye pointi 29 wakati Yanga Princess ina pointi 22 na kwenye msimamo ni ya tano.



Wanariadha wa klabu mbalimbali za mkoa wa Dar es Salaam, wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Taifa jijini ili kujiandaa na mashindano ya taifa yanayotarajiwa kufanyika Septemba, mwaka huu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Namungo yaitangazia vita Sahare FA*

**Na Adam Fungamwango**

NAMUNGO FC imesema inaionea huruma Sahare All Stars kwa 'kupotea njia' kutokana na kichapo watakapokutana katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayofanyika Julai 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

Ofisa Habari wa Namungo FC, Kindamba Namlia, aliliambia gazeti hili kwa sasa hawafikirii kabisa mechi hiyo na mashabiki wao wanauwaza mchezo wa fainali utakaochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga.

"Ni kweli mashabiki wetu watakwenda mjini Tanga kutupa hamasa, lakini wengi zaidi wamesema wao wamejiandaa zaidi kwenda Sumbawanga kwa sababu wanajua kikosi chetu hakiwezi kusumbuliwa na wenyeji wetu," alisema Namlia.

Kiongozi huyo alisema lengo la Namungo msimu huu ni kuona timu hiyo inakata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa na si vinginevyo.

"Tumejipanga kisawasawa, ni kama mtu aliyeamua kufanya kazi ya kuchinja, ina maana akiwa machinjioni kitu kitakacholetewa na mteja basi tunachinja tu, hatuangalii rangi wala saizi, Sahare wamekuja, ni bahati mbaya sana kwao. Tunachofanya kwa sasa ni kuwakatia pasipoti wachezaji wetu ambao hawana kwa ajili ya kusafiri kuelekea mechi za kimataifa," alisema ofisa huyo.

Safari ya Namungo kwenye michuano hiyo inayotoa mwakilishi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), ilianza kwa kuichapa Might Elephants bao 1-0, halafu wakawafunga Green Warrios goli 1-0 baadaye wakaiadhibu Biashara United mabao 2-0 na kuifunga Mbeya City mabao 2-1 na kuwachapa Alliance goli 1-0.

Timu hiyo pia imekuwa ikifanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kucheza mechi 16 sasa bila kupoteza, ikishika nafasai ya nne katika msimamo ikiwa na pointi 56.

# Michezo

Jumamosi Julai 4, 2020

Nipashe




Bayern rasmi yamsajili Sane UKURASA 22

# Mechi chungu Yanga Ligi Kuu Bara

●●● Ilianzia katika mechi ya ufunguzi dhidi ya Ruvu Shooting, sare ziliwaandama huku Zahera akichelewa...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya tatu, Yanga imekosa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kushuhudia taji hilo likienda kwa watani zao, Simba, huku sababu kubwa msimu huu ikionekana ni kukosa maandalizi ya mwanzo wa msimu, kutofanya vema mechi za mwanzo na kupata sare nyingi zilizovunja rekodi.

**Kutoshinda mechi mbili za mwanzo tu, zilitosha kabisa kuifanya Yanga kuanza kuondoka taratibu kwenye kinyang'anyiro cha kuwania ubingwa wa msimu huu wa 2019/20, hasa ikizingatiwa Simba walishinda mechi hizo za mwanzo.**

Yanga ilifungua msimu kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting hapo Agosti 26, mwaka jana huu na Oktoba 3, ilitoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Polisi Tanzania.

Mechi hizi mbili tu, ziliifanya Yanga kubaki na pointi moja tu, huku Simba ikiwa tayari imeshakusanya pointi sita kwa kuifunga JKT Tanzania mabao 3-1 kwenye mechi ya kwanza waliyocheza Agosti 29, mwaka jana na pia kuitwanga Mtibwa Sugar mabao 2-1, Septemba 13, mwaka jana.

Hii ilitokana na wachezaji wa timu hiyo kutofanya vizuri maandalizi ya kuanza kwa msimu maarufu kama 'Pre-season' iliyokuwa mjini Morogoro ikisimamiwa kwa muda mrefu wa Kocha Msaidizi, Noel Mwandila, huku Kocha Mkuu Mkongomani, Mwinyi Zahera akiwa nchini Ufaransa kwa mapumziko.

Hili ndilo linaonekana tatizo kubwa la msingi, kwani hata aliporejea, ilibaki wiki moja tu kabla ya michuano ya kimataifa Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini pia Ligi Kuu Bara ikiwa imekaribia.

Zahera (pichani) alionekana kutokuwa tena na muda wa kuwaandaa wachezaji, bali ni kuwapa mazoezi ya kawaida tu kwa ajili ya michuano iliyokuwa imekaribia.



Sababu nyingine ya Yanga kuukosa ubingwa msimu huu ni sare zilizopitiliza. Kwa mara ya kwanza tangu mfumo mpya wa Ligi Kuu Bara uanze msimu wa 2007/08, Yanga haijawahi kufikisha idadi kubwa ya sare kama msimu huu.

Kabla ya hata msimu haujamalizika, ikiwa imebakisha mechi sita, tayari Yanga ina sare 12 ambazo ni rekodi ya klabu.

Mara ya mwisho Yanga kupata sare nyingi kwa msimu mmoja, ilikuwa ni msimu wa 2017/18, ilipopata sare 10, na hata msimu uliopita ambapo ilionekana timu ni dhaifu zaidi chini ya Zahera, ilitoa sare tano tu.

Wakati Yanga ikiwa na idadi hiyo, Simba imetoa sare nne tu mpaka sasa. Hizo ni idadi ya sare ambazo Yanga ilitoka mfululizo msimu huu dhidi ya Mbeya City bao 1-1, sare ya bila kufungana dhidi ya Prisons, ikatoka sare tena ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania na suluhu nyingine dhidi ya Coastal Union.

Hata Simba ilipokuwa ikipoteza mechi zake hizo chache, Yanga yenyewe ilikuwa ikitoa sare na ilipokuwa ikishinda, bado Yanga iliendelea na sare zake au kufungwa.

Kutokuwa na mwendelezo mzuri wa mechi za ushindi pia kumekuwa msaada mkubwa kuinyima Yanga ubingwa msimu huu, kwani haikuwa ikishinda mechi nyingi mfululizo kama watani zao wa jadi, Simba.

Mechi nyingi mfululizo ambazo Yanga imeshinda ni tano tu, lakini baada ya hapo inacheza mechi mbili, inatoka sare, au mechi nne, inafungwa.

Wakati ikisuasua, Simba imeshinda mechi sita mfululizo mara mbili. Ilishinda mechi sita, ikafungwa bao 1-0 dhidi ya Mwadui FC, lakini ikashinda tena mechi sita mfululizo, ndipo ikapoteza dhidi ya Yanga kwa bao 1-0.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa Namungo kuwaalika JKT Tanzania wakati Kagera Sugar itacheza dhidi ya Ruvu Shooting huku Singida United ikiwafuata Azam FC, KMC wao watapambana na Mwadui FC na Mbao watawakaribisha Lipuli.

Kwenye Uwanja wa CCM Sokoine wenyeji Tanzania Prisons watawaalika Polisi Tanzania huku kesho Ndanda ikicheza dhidi ya mabingwa, Simba na Biashara United itawakaribisha Yanga kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma.



Golikipa wa Manchester City, Ederson (chini), akipambana kumzuia mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, asifunge katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. City ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yafuata heshima Kusini

**Na Saada Akida**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, waliwasili salama Mtwara na kuendelea na maandalizi ya kuwavaa Ndanda FC katika mchezo wa raundi ya 33 utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani humo.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili kuwa pamoja na kuwa wameshatetea ubingwa, watashuka uwanjani kuikabili Ndanda wakidhamiria kupata ushindi na si kukamilisha ratiba.

Rweyemamu alisema kila mchezo kwao ni muhimu na watashuka uwanjani wakifahamu wenyeji wao wanahitaji ushindi ili kujiondoa kwenye janga la kushuka daraja.

"Tunahitaji ushindi, tunahitaji kuupa heshima ubingwa wetu, tutacheza kwa nguvu ile ile ya mwanzoni," alisema kwa kifupi meneja huyo.

Baada ya mchezo huo, Simba itaeelekea Lindi kwa ajili ya kuwavaa Namungo FC katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa.

Mabingwa hao wanatarajia kukabidhiwa kombe baada ya kutwaa ubingwa kwa msimu wa 2019/20 na kombe hilo litakuwa ni la kwao jumla kwa sababu ya kulitwaa mara tatu mfululizo.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042